BENKI KUU YA TANZANIA



Tathmini Ya Mwenendo Wa Uchumi

Oktoba 2026


Yaliyomo

1.0 Mwenendo wa Uchumi wa Dunia....1
2.0 Mwenendo wa Uchumi wa Taifa....3
2.1 Mfumuko wa Bei....3
2.2 Sera ya Fedha....6
2. 3 Viwango vya Riba....8
2. 5 Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali....10
2.6 Mwenendo wa Deni la Taifa....11
2.7 Mwenendo wa Sekta ya Nje....13
3.0 Mwenendo wa Uchumi wa Zanzibar....16
3.1 Mfumuko wa Be....16
3.2 Bajeti ya Serikali....16
3.3 Mwenendo wa Sekta ya Nje....17
VIAMBATISHO....19

1.0 Mwenendo wa Uchumi wa Dunia


Uchumi wa dunia umeendelea kuwa stahimilivu,ingawa matarajio ya ukuaji wake yanatofautiana miongoni mwa kanda. Kutokana na mwelekeo huo, taarifa ya Shirika la Fedha la Kimataifa ya Oktoba 2026, inakadiria ukuaji wa uchumi wa dunia kwa mwaka 2026 kuwa asilimia 3.1, ambao ni zaidi ya maoteo ya asilimia 3 ya mwezi Julai 2026[1]. Marekebisho hayo ya makadirio yanatokana na ustahimilivu wa mahitaji ya ndani, uwezo wa sekta binafsi kuhimili mabadiliko ya mazingira ya kiuchumi, pamoja na uwekezaji kwenye teknolojia ya akili unde, ambayo yanatarajiwa kupunguza athari za misukosuko ya soko la nishati itokanayo na mgogoro wa Mashariki ya Kati. Uchumi kwenye nchi zilizoendelea unatarajia kukua kwa asilimia 2.1, ukichangiwa zaidi na Marekani. Kwa upande mwingine, ukuaji wa nchi zinazoibukia na zinazoendelea kiuchumi unatarajiwa kufikia asilimia 3.7, ukichagizwa zaidi na kasi kubwa ya ukuaji nchini India uliofidia kupungua kwa makadirio ya ukuaji wa China. Makadirio ya ukuaji wa uchumi Kusini mwa Jangwa la Sahara yameongezeka hadi asilimia 4.5 kutoka asilimia 4.3 ya mwezi Julai 2026, yakichochewa na kuimarika kwa urari wa biashara kwa nchi zinazouza mafuta. Hata hivyo, nchi zinazoagiza mafuta zinaendelea kukabiliwa na ongezeko la gharama ya nishati, pamoja na manufaa madogo yanayotokana na ukuaji wa teknolojia ya akili unde. Kwa ujumla, mtazamo juu ya sera za uchumi wa dunia umeendelea kuwa wa tahadhari, licha ya kuimarika kwa mazingira ya biashara duniani (Kielelezo 1.1a na Kielelezo 1.1b).

Kielelezo 1.1a: Fahirisi ya Kutotabirika kwa Sera za Uchumi wa Dunia



Chanzo: Fahirisi ya Kutokuwa na Uhakika wa Sera za Uchumi Duniani, Septemba 2026 (https://worlduncertaintyindex.com/)

Kielelezo 1.1b: Fahirisi ya Kutotabirika kwa Biashara Duniani



Chanzo: Fahirisi ya Kutokuwa na Uhakika wa Sera za Uchumi Duniani, Septemba 2026 https://worlduncertainityindex.com/


Bei za bidhaa katika soko la dunia zilikuwa na mienendo tofauti kwa mwezi Septemba 2026. Bei ya nishati iliongezeka kwa kasi, kufikia wastani wa dola za Marekani 102.3 kwa pipa, kutoka dola za Marekani 84.4 mwezi Agosti 2026, kufuatia kuendelea kwa mgogoro Mashariki ya Kati. Wakati huo huo, kupungua kwa mahitaji ya dhahabu kama hifadhi salama ya thamani yalishusha bei hadi wastani wa dola za Marekani 4,319 kwa wakia, kutoa dola za Marekani 4,411 mwezi uliotangulia.

Bei za bidhaa za kilimo zikiwemo ngano, mahindi na mchele ziliongezeka kutokana na changamoto za usafirishaji katika eneo la Bahari Nyeusi pamoja na hali mbaya ya hewa katika baadhi ya maeneo ya Amerika ya Kaskazini. Bei ya mafuta

[1] Marekebisho ya kuongeza makadirio yanaendana na mtazamo wa hivi karibuni wa Shirika la Ushirikiano wa Kiuchumi na Maendeleo (OECD), ambalo katika ripoti yake ya Septemba 2026 liliongeza makadirio ya ukuaji wa uchumi kwa mwaka 2026 hadi asilimia 2.9, kutoka asilimia 2.8 katika ripoti ya Juni 2026.

ya mawese iliimarika, ikichangiwa na ongezeko kubwa la mahitaji na hatari za kupungua kwa uzalishaji kutokana na hali ya El Niño. Vilevile, bei ya sukari iliongezeka kufuatia matarajio ya kupungua kwa ugavi kutoka Thailand na India. Kutokana na kuimarika kwa ugavi katika soko la dunia, bei za kahawa zilipungua. Aidha, bei za mbolea ziliongezeka kwa kiwango cha wastani, ambapo bei za Urea na DAP zilipanda kutokana na kuendelea kuwepo kwa changamoto za ugavi zinazohusishwa na mgogoro wa Mashariki ya Kati pamoja na uhaba wa pembejeo katika soko (Kielelezo 1.2, Jedwali 1.1 na Kiambatisho A8).

Kielelezo 1.2: Bei za Bidhaa Katika Soko la Dunia



Chanzo: Bloomberg

Jedwali 1.1: Bei ya Bidhaa Katika Soko la Dunia Wastani kwa kila mwezi

Bidhaa	Kipimo	Ago-26	Sep-26	Badiliko (%)
Mafuta ghafi	Dola ya Marekani/pipa	84.4	102.3	21.2
Dhahabu	Dola ya Marekani/wakia	4,411	4,319	-2.1
Gesi asilia	Dola ya Marekani/mmbtu	21.11	25.42	20.4
Ngano	Dola ya Marekani/tani	330	347	5.2
Sukari	Dola ya Marekani/kg	0.38	0.41	7.9
Kahawa, Arabica	Dola ya Marekani/kg	7.97	7.26	-8.9
Kahawa, Robusta	Dola ya Marekani/kg	3.98	3.69	-7.3
Mafuta ya mawese	Dola ya Marekani/tani	1,132	1,180	4.2
DAP (mbolea)	Dola ya Marekani/tani	793.5	800.6	0.9
Urea (mbolea)	Dola ya Marekani/tani	390.0	408	4.5

Chanzo: Takwimu za Bei za Bidhaa za Benki ya Dunia Septemba 2026.

Tanbihi: DAP inamaanisha fosfeti ya diamoniamu mmbtu ni milioni ya vipimo vya joto vya Uingereza

Mfumuko wa bei duniani uliendelea kuwa juu katika nchi nyingi mwezi Septemba 2026, ukichangiwa na ongezeko la bei ya nishati kufuatia mgogoro unaoendelea Mashariki ya Kati. Kupanda kwa gharama za mafuta kulisababisha ongezeko la gharama za usafirishaji, huduma za umeme na maji, pamoja na gharama za uzalishaji, hali iliyochochea upya shinikizo la mfumuko wa bei katika nchi mbalimbali. Mfumuko wa bei kwa nchi zilizoendelea, hususan Marekani na Ukanda wa Ulaya uliongezeka kutokana na kupanda kwa bei ya nishati kufuatia kukosekana kwa utulivu Mashariki ya Kati. Ongezeko hilo la mfumuko wa bei lilizifanya Benki Kuu kubwa duniani kuashiria uwezekano wa kutekeleza sera ya fedha inayodhibiti zaidi ukwasi endapo shinikizo la bei litadumu (Kielelezo 1.3).

Katika nchi zinazoibukia kiuchumi na zinazoendelea, mienendo ya mfumuko wa bei ilikuwa tofauti, ingawa kwa ujumla ilionekana kupanda. Mfumuko wa bei uliongezeka nchini India kutokana na hali mbaya ya hewa inayohusiana na mvurugiko wa mnyororo wa ugavi pamoja na bei kubwa za mafuta. Nchini China, ongezeko la mfumuko wa bei lililotokana na kuongezeka kwa gharama za nishati likifidiwa kwa kiasi na kushuka kwa bei za vyakula.

Kielelezo 1.3: Mfumuko wa Bei kwa Nchi Zinazoendelea na Zinazoibukia Kiuchumi

Asilimia



Chanzo: Bloomberg

Mwenendo wa mfumuko wa bei katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika ulitofautiana, ingawa nchi nyingi ziliendelea kubaki ndani ya vigezo vya mtangamano wa kikanda (Kielelezo 1.4 na Kielelezo 1.5).

Kwa upande wa Tanzania, kuendelea kuwa juu kwa bei za nishati na mbolea katika soko la

dunia kunaweza kuathiri mwelekeo wa uchumi kwa kuongeza gharama za uagizaji wa bidhaa kutoka nje na kuchochea shinikizo la mfumuko wa bei hapa nchini. Hali hii inaweza kulazimu kutekelezwa kwa sera ya fedha inayodhibiti zaidi ukwasi. Hata hivyo, kuimarika kwa bei ya mazao ya kilimo pamoja na kuongezeka kwa mahitaji ya kikanda kunatarajiwa kuongeza mapato yatokanayo na mauzo ya nje na kuchochea shughuli za kiuchumi

Kielelezo 1.4: Mfumuko wa Bei kwa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki


Asilimia



Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu
Tanbihi: Mistari ya nukta inaashiria viwango vya mfumuko wa bei vilivyokusudiwa

Kielelezo 1.5: Mfumuko wa Bei Miongoni mwa Nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika

Asilimia



Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu
Tanbihi: Mistari ya nukta inaashiria viwango vya mfumuko wa bei vilivyokusudiwa

Hatari za kudorora kwa uchumi wa dunia zinaendelea kuwa kubwa. Mgogoro wa muda mrefu Mashariki ya Kati unaweza kuvuruga masoko ya nishati na njia za biashara za kimataifa, kudhoofisha matarajio ya ukuaji wa uchumi, na kuongeza shinikizo la mfumuko wa bei.

Aidha, hatari za mabadiliko ya tabia nchi bado ni kubwa, huku hali ya El Niño ikiendelea kuhatarisha uzalishaji kwenye kilimo na upatikanaji wa chakula. Hali ya hewa isiyoridhisha inaweza kusababisha upungufu wa upatikanaji wa chakula na kusababisha ongezeko la bei za vyakula.

2.0 Mwenendo wa Uchumi wa Taifa

2.1 Mfumuko wa Bei

Mfumuko wa bei wa mwaka uliendelea kubaki ndani ya wigo wa lengo la kitaifa la asilimia 3 hadi 5 ukibakia asilimia 4.3 mwezi Septemba 2026, sawa na mwezi Agosti 2026 (Jedwali 2.1.1 na Kielelezo 2.1.1). Utulivu huu ulichangiwa na kupungua kwa mfumuko wa bei wa nishati, mafuta na huduma za msingi, ambao kwa kiasi umefidia ongezeko katika mfumuko wa bei wa chakula.

Mfumuko wa bei unatarajiwa kuendelea kuwa katika kiwango cha juu kwa miezi ijayo, kutokana na kuendelea kwa mgogoro wa Mashariki ya Kati na matarajio ya mvua zinazotokana na hali za El Niño kipindi cha msimu wa Vuli. Licha ya mashinikizo haya, mfumuko wa bei unatarajiwa kuendelea kubaki ndani ya lengo la kitaifa na vigezo vya mtangamano wa kikanda, ukichangiwa kwa kiasi kikubwa na ziada ya chakula kilichozalishwa kwenye msimu wa mavuno wa 2025/26.

Jedwali 2.1.1: Mwenendo wa Mfumuko wa Bei


Asilimia (Kizio: 2020 = 100)

		Badiliko la Mfumuko wa bei (Asilimia)					
		Badiliko: Mwezi hadi Mwezi			Badiliko kwa Mwaka		
Makundi Makuu ya Fahirisi	Mizania	Sep-25	Ago-26	Sep-26	Sep-25	Ago-26	Sep-26
Vyakula na Vinywaji Baridi	28.2	-0.6	-0.3	-0.5	7.0	3.7	3.9
Vinywaji Vikali na Tumbaku	1.9	0.6	0.0	0.2	3.6	1.5	1.1
Nguo, Mavazi na Viatu	10.8	0.3	0.2	0.1	1.9	1.8	1.7
Makazi, maji, umeme, gesi na nishati zinginezo	15.1	0.3	0.3	0.3	2.3	2.5	2.5
Samani, Vifaa vya Nyumbani na Ukarabati wa Makazi	7.9	0.6	0.4	0.5	2.8	2.6	2.6
Afya	2.5	0.0	0.0	0.0	1.2	1.5	1.4
Usafiri	14.1	0.9	0.1	1.1	2.1	13.8	14.0
Habari na Mawasiliano	5.4	0.0	0.9	0.0	0.2	1.5	1.5
Burudani, Michezo na Utamaduni	1.6	-0.1	0.2	-0.3	0.8	0.7	0.5
Elimu	2.0	0.0	0.2	0.0	2.9	3.2	3.2
Migahawa na Huduma za Malazi	6.6	0.1	0.2	0.0	1.0	3.0	2.9
Bima na Huduma za Kifedha	2.1	0.0	0.0	0.0	0.4	0.2	0.2
Huduma Binafsi, Hifadhi ya Jamii na Bidha na Huduma Mchanganyiko	2.1	0.0	0.0	0.0	2.3	3.3	3.3
Fahirisi Bidhaa Zote	100.0	0.1	0.1	0.1	3.4	4.3	4.3
Makundi Mengine Teule							
Faharisi ya Bidhaa za Msingi	73.9	0.3	0.3	0.4	2.2	4.1	4.1
Fahirisi Isiyojumuisha Fahirishi za Bidhaa za Msingi	26.1	-0.5	-0.4	-0.5	6.7	4.8	4.9
Fahirisi za Mafuta, Nishati na Bili za Maji	5.7	0.9	0.1	0.2	3.7	8.5	7.8
Fahirisi za Huduma	37.2	0.4	0.2	0.6	1.3	5.9	6.1
Fahirisi za Bidhaa	62.8	-0.1	0.0	-0.2	4.7	3.5	3.4
Fahirisi za Bidhaa na Huduma za Elimu	4.1	0.1	0.2	0.0	2.5	1.8	1.7
Fahirisi za Bidhaa zote Isipokuwa Chaakula na Vinywaji Visivyo na Kilevi	71.8	0.4	0.2	0.4	1.9	4.6	4.6

Chanzo: Ofisi ya taifa ya Takwimu na Uchambuzi wa Benki Kuu ya Tanzania

Kielelezo 2.1.1: Mfumuko wa Bei na Malengo yake


Asilimia



Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Uchambuzi wa Benki Kuu ya Tanzania.

Mfumuko wa bei wa bidhaa za msingi (usiojumuisha bei za vyakula visivyochakatwa na nishati) ulibakia kuwa asilimia 4.1 mwezi Septemba 2026, sawa na mwezi uliotangulia, ingawa ulikuwa juu ya asilimia 2.2 iliyorekodiwa mwezi kama huo mwaka 2025. Mfumuko wa bei kwenye makundi mengine ikiwemo mavazi na viatu, na huduma za afya na elimu uliendelea kuwa tulivu au kupungua, huku mfumuko wa bei wa usafirishaji uliongezeka (Jedwali 2.1.1 na Kielelezo 2.1.2).

Kielelezo 2.1.2: Viwango vya Mfumuko wa Bei kwa Miezi Kumi na Mbili




Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Uchambuzi wa Benki Kuu ya Tanzania

Mfumuko wa bei wa bidhaa za msingi (usiojumuisha bei za vyakula visivyochakatwa na nishati) ulibakia kuwa asilimia 4.1 mwezi Septemba 2026, sawa na mwezi uliotangulia, ingawa ulikuwa juu ya asilimia 2.2 iliyorekodiwa mwezi kama huo mwaka 2025. Mfumuko wa bei kwenye makundi mengine ikiwemo mavazi na viatu, na huduma za afya na elimu uliendelea kuwa tulivu au kupungua, huku mfumuko wa bei wa usafirishaji uliongezeka (Jedwali 2.1.1 na Kielelezo 2.1.2).

Kielelezo 2.1.2: Viwango vya Mfumuko wa Bei kwa Miezi Kumi na Mbili

Asilimia




Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Uchambuzi wa Benki Kuu ya Tanzania.

Mfumuko wa bei ya chakula uliongezeka kufikia asilimia 3.9 mwezi Septemba 2026, kutoka asilimia 3.7 ya mwezi uliotangulia, na chini ya asilimia 7 ya mwezi kama huo mwaka 2025. Ongezeko hili lilichangiwa na kuongezeka kwa bei za mtama,

viazi, ulezi na ngano (Kielelezo 2.1.3a na Kielelezo 2.1.3b).


Kielelezo 2.1.3: Mabadiliko ya Mwaka ya Bei za Jumla za Mazao

a. Mazao ya Vyakula Vikuu



Chanzo: Wizara ya Viwanda na Biashara, na Uchambuzi wa Benki Kuu ya Tanzania

b. Mazao ya Vyakula Mbadala



Chanzo: Wizara ya Viwanda na Biashara, na Uchambuzi wa Benki Kuu ya Tanzania

Akiba ya chakula iliyohifadhiwa na Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula ilifikia tani 478,160.6, baada ya kununua tani 705.7 na kuuza tani 6,877.1 za mahindi na mpunga kwa wafanyabiashara mbalimbali (Jedwali 2.1.2).

Jedwali 2.1.2: Akiba ya Chakula Iliyohifadhiwa na Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula


Tani

Kipindi	2022	2023	2024	2025	2026
Jan	207,899	124,736	270,984	646,480	567,469
Feb	203,297	106,881	326,172	619,659	560,008
Mac	200,626	80,123	336,099	587,062	533,634
Apr	190,366	63,808	340,102	557,228	510,927
Mei	149,402	51,367	340,002	509,990	500,692
Jun	141,576	46,665	340,479	477,923	489,998
Jul	140,695	94,088	368,855	485,930	487,056
Ago	144,410	210,020	489,187	537,571	484,332
Sep	149,044	244,169	651,403	570,519	478,160
Okt	151,794	244,289	708,399	593,485	
Nov	147,401	244,223	702,502	590,425	
Des	137,655	248,282	677,115	577,376	

Chanzo: Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula

Mfumuko wa bei ya nishati, mafuta na huduma za msingi ulipungua hadi asilimia 7.8 mwezi Septemba 2026, kutoka asilimia 8.5 ya mwezi Agosti 2026. Ingawa ulibakia juu ya asilimia 3.7 iliyorekodiwa mwezi kama huo mwaka 2025. Kupungua huko kuliakisiwa kwa kiasi kikubwa na bei za petroli, dizeli, na mafuta ya taa (Jedwali 2.1.1 na Kielelezo 2.1.4).

Kielelezo 2.1.4: Bei za Bidhaa za Mafuta Kwa lita




Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu
Tanbihi: Bidhaa nyeupe za petroli huashiria wastani wa bei za Dunia

Mfumuko wa bei wa bidhaa za msingi uliendelea kuwa na mchango mkubwa kwenye mfumuko wa bei wa jumla, ukichangia asilimia 3.1 mwezi Septemba 2026 ikilinganishwa na mchango wa asilimia 1.6 kipindi kama hicho mwaka 2025 (Kielelezo 2.1.5).

Kielelezo 2.1.5: Mchango Katika Mfumuko wa Bei

Asilimia



Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Uchambuzi wa Benki Kuu ya Tanzania


2.2 Sera ya Fedha

Utekelezaji wa sera ya fedha uliendelea kufanyika kwa mujibu wa maamuzi ya Kamati ya Sera ya Fedha ambayo yalipelekea ongezeko la Riba ya Benki Kuu hadi asilimia 6.25 kwa robo mwaka iliyoishia Septemba 2026 kutoka asilimia 5.75 kwa robo mwaka iliyotangulia. Uamuzi huu ulilenga kudhibiti shinikizo la mfumuko wa bei la duru ya pili ambao ungeweza kusababishwa na athari zinazotokana na kuongezeka kwa gharama ya nishati, mbolea na usafirishaji. Sambamba na hilo, utekelezaji wa sera ya fedha ulilenga kuhakikisha kuwa riba ya mikopo ya siku saba baina ya mabenki inabaki ndani ya wigo wa asilimia 4.75 hadi asilimia 7.75.

Kufuatia utekelezaji madhubuti wa sera ya fedha, ukwasi katika mfumo wa kibenki uliendelea kuwa wa kutosha mwezi Septemba 2026, huku riba ya mikopo ya siku saba katika soko la fedha baina ya mabenki ikiendelea kubaki ndani ya wigo (Kielelezo 2.2.1). Utekelezaji wa sera ya fedha ulifanyika zaidi kupitia mikopo ya muda mfupi na nyenzo za kudhibiti ukwasi. Kufuatia uwepo wa ukwasi wa kutosha katika mfumo wa kibenki, mahitaji ya mikopo ya muda mfupi yalipungua, hadi shilingi bilioni 2,624.5 ikilinganishwa na shilingi bilioni 3,037.4 mwezi uliotangulia (Kielelezo 2.2.2).


Kielelezo 2.2.1: Riba ya Benki Kuu na Wastani wa Siku 5 wa Riba ya Mikopo ya Siku 7

Asilimia



Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania


Kielelezo 2.2.2: Mikopo ya Muda Mfupi Kwa Mabenki



Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

Ukuaji wa ujazi wa fedha na mikopo kwa sekta binafsi uliendelea kuwa imara, hali inayoashiria kuimarika kwa shughuli za kiuchumi hapa nchini pamoja na kuendelea kuwepo kwa mahitaji ya mikopo. Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana ulikua kwa asilimia 25.9 katika mwaka ulioishia Septemba 2026, ukichagizwa na ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi wa asilimia 34.2 (Kielelezo 2.2.3, 2.2.4 na 2.2.5 na Jedwali 2.2.1). Ukuaji huo mkubwa wa mikopo uliendelea kuashiria kuongezeka kwa mahitaji ya fedha za uwekezaji, kutokana na upanuzi wa shughuli za biashara pamoja na ustahimilivu wa uchumi kwa ujumla.

Kielelezo 2.2.3: Mwenendo wa Ujazi Wa Fedha




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

Jedwali 2.2.1: Ujazi wa Fedha na Vipengele Vyake

	Kiasi (Shilingi Bilioni)			Ukuaji kwa mwaka (%)		
Kipengele	Sep-25	Ago-26	Sep-26	Sep-25	Ago-26	Sep-26
Rasilimali halisi za nje	15,896.7	13,575.4	13,152.3	16.0	-13.9	-17.3
Rasilimali halisi za nje za Benki Kuu	14,467.3	13,730.9	14,139.1	13.0	-1.5	-2.3
Rasilimali halisi za nje za mabenki	1,429.3	-155.5	-986.7	---	---	---
Rasilimali halisi za ndani	41,957.4	58,553.3	59,675.6	22.1	40.4	42.2
Madai rasmi ya ndani	54,854.2	68,093.2	69,436.3	16.3	24.8	26.6
Dhamana za Serikali zilizonunuliwa na benki za biashara	8,723.1	11,718.3	12,056.9	6.8	40.3	38.2
Mikopo kwa sekta binafsi	41,999.9	55,255.9	56,359.4	16.1	33.0	34.2
Rasilimali nyinginezo	-12,896.9	-9,539.8	-9,760.7	0.8	-25.9	-24.3
Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3)	57,854.0	72,128.7	72,827.9	20.4	25.5	25.9
Amana za fedha za kigeni	13,337.2	16,043.5	15,493.3	7.3	17.1	16.2
Ujazi wa fedha, kwa tafsiri pana (M2)	44,516.8	56,085.2	57,334.6	24.9	28.2	28.8
Amana zinginezo	16,600.4	20,492.4	21,212.9	20.2	25.3	27.8
Ujazi wa fedha, kwa tafsiri finyu (M1)	27,916.4	35,592.8	36,121.8	27.9	29.9	29.4
Ujazi wa fedha ulio kwenye mzunguko	7,730.8	9,119.9	9,394.0	5.1	13.5	21.5
Amana za hundi	20,185.6	26,472.9	26,727.7	39.5	36.7	32.4
Fedha za msingi (M0)	13,717.6	17,245.9	17,127.7	23.2	27.4	24.9


Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

Kielelezo 2.2.4: Mabadiliko Katika Vyanzo vya Ujazi wa Fedha kwa Mwaka



Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

Kielelezo 2.2.5: Mwenendo Wa Mikopo Kwa Sekta Binafsi



Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania na mabenki

Ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi uliendelea kuonekana katika shughuli nyingi za kiuchumi, ambapo shughuli za uchukuzi na mawasiliano zilirekodi ukuaji wa juu zaidi, zikifuatiwa na biashara na kilimo (Jedwali 2.2.2). Mikopo kwa ajili ya shughuli binafsi ambayo kwa kiasi kikubwa hutumika kugharamia shughuli za jasiriamali ndogo sana, ndogo na za kati iliendelea kuchukua sehemu kubwa ya mikopo yote ikiwa na asilimia 33.9, ikifuatiwa na shughuli za biashara na kilimo kwa asilimia 15.6 na asilimia 13.7, mtawalia (Kielelezo 2.2.6).

Jedwali 2.2.2: Ukuaji wa Mikopo kwa Shughuli za Kiuchumi


Asilimia

	Sep-25	Apr-26	Mei-26	Jun-26	Jul-26	Ago-26	Sep-26
Uchukuzi na mawasiliano	17.4	39.7	44.6	59.5	66.0	77.2	78.3
Biashara	24.8	44.2	35.0	46.4	43.5	47.1	52.5
Kilimo	27.6	30.5	30.9	30.1	37.3	38.4	41.9
Uchimbaji Madini	32.4	39.7	19.8	39.9	65.2	75.9	35.2
Ujenzi	15.7	20.6	25.4	34.4	38.9	41.8	34.3
Hoteli na migahawa	16.3	6.0	-2.9	0.9	25.1	24.6	32.7
Shughuli binafsi	14.7	17.7	20.0	21.8	24.7	24.9	23.1
Viwanda	0.1	4.2	3.3	8.3	5.1	12.9	17.7

Chanzo: Mabenki na Uchambuzi wa Benki Kuu ya Tanzania

Kielelezo 2.2.6: Mgawanyo wa Mikopo Katika Shughuli za Kiuchumi

Asilimia



Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

2. 3 Viwango vya Riba

Mwenendo wa viwango vya riba uliakisi mwelekeo wa sera ya fedha. Wastani wa riba za mikopo uliongezeka kidogo hadi asilimia 15.54 mwezi Septemba 2026, kutoka asilimia 15.05 mwezi uliotangulia. Riba za mikopo kwa wateja wakubwa ziliongezeka hadi asilimia 12.03 kutoka asilimia 11.93 mwezi Agosti 2026. Wastani wa riba za amana uliongezeka hadi asilimia 9.02, kutoka asilimia 8.78 mwezi uliotangulia. Wakati huo huo, riba za amana kwa wateja wakubwa zilikuwa asilimia 11 karibu sawa na mwezi uliotangulia. Kutokana na mwenendo huo, wigo kati ya riba za mikopo na amana za mwaka mmoja ulipungua hadi asilimia 5.78 kutoka asilimia 5.95 (Jedwali 2.3.1).

Jedwali 2.3.1: Riba za Amana na Mikopo inayotolewa na Benki za Biashara

Asilimia

	Mac-26	Apr-26	Mei-26	Jun-26	Jul-26	Ago-26	Sep-26
Riba za amana	2.89	2.91	2.85	2.90	2.90	2.77	2.95
Riba ya mikopo - jumla	15.11	15.33	15.32	15.22	15.10	15.05	15.54
Riba za mikopo (mwaka 1)	15.45	15.31	15.38	15.38	15.54	15.31	15.36
Riba za mikopo (wateja wakubwa)	12.21	12.56	11.90	11.93	12.04	11.93	12.03
Riba za amana -jumla	8.33	8.54	8.43	8.69	8.78	8.78	9.03
Riba za amana (miezi 12)	9.60	9.81	10.17	9.72	9.34	9.36	9.59
Riba za amana (wateja wakubwa)	11.57	11.37	11.25	11.17	10.99	11.06	11.00
Tofauti kati ya riba za mikopo na amana	5.85	5.50	5.22	5.66	6.20	5.95	5.78


Chanzo: Mabenki na Uchambuzi wa Benki Kuu ya Tanzania

2.4 Masoko ya Fedha

Soko la dhamana za Serikali

Soko la dhamana za Serikali liliendelea kuwa na ufanisi mwezi Septemba 2026, likichochewa na mahitaji makubwa ya wawekezaji pamoja na uwepo wa ukwasi wa kutosha katika uchumi. Katika kipindi hicho, Benki ilifanya minada miwili ya dhamana za Serikali za muda mfupi yenye thamani ya shilingi bilioni 678.3, kwa ajili ya kugharamia matumizi ya Serikali na utekelezaji wa sera ya fedha. Minada yote ilikuwa na mahitaji makubwa kuliko ilivyopangwa ikipokea zabuni zenye thamani ya shilingi bilioni 1,205, ambapo zabuni zenye thamani ya shilingi bilioni 654.6 zilikubaliwa. Licha ya ongezeko la mahitaji hayo, wastani wa riba ya dhamana za Serikali za muda mfupi ulibaki kuwa asilimia 4.85 mwezi Septemba 2026 (Kielelezo 2.4.1).

Kielelezo 2.4.1: Mwenendo wa Minada ya Dhamana za Serikali




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

Benki ilifanya minada ya hati fungani za miaka 5, 10 na 15, zenye thamani ya shilingi bilioni 145.6, 182.9 na shilingi bilioni 207.3, mtawalia. Minada yote ilikuwa na mahitaji makubwa kuliko ilivyopangwa, ikipokea jumla ya zabuni zenye thamani ya shilingi bilioni 1,267.2, ambapo zabuni zenye thamani ya shilingi bilioni 489.7 zilikubaliwa. Kutokana na mahitaji hayo, riba za hati fungani za miaka 5 na 10 zilipungua hadi asilimia 9.53 na 10.69, mtawalia, huku riba ya hatifungani ya miaka 15 ikibaki asilimia 10.79.

Soko la fedha baina ya mabenki

Soko la fedha baina ya mabenki liliendelea kuwa nyenzo muhimu ya kusambaza ukwasi miongoni mwa mabenki, hali iliyochangia matokeo ya sera ya fedha kuonekana kwenye riba za muda mfupi. Kwa mwezi Septemba 2026, mauzo katika soko yaliongezeka hadi shilingi bilioni 4,791.7, kutoka shilingi bilioni 4,566.2 mwezi uliotangulia. Mikopo ya siku saba iliendelea kuchukua sehemu kubwa, takriban asilimia 62 ya mauzo yote katika soko. Wakati huohuo, wastani wa riba katika soko la fedha baina ya mabenki ulibaki asilimia 6.67, sawa na kiwango kilichorekodiwa mwezi Agosti 2026 (Kielelezo 2.4.2).

Kielelezo 2.4.2: Mwenendo wa Soko la Fedha




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

Soko la fedha za kigeni

Mwezi Septemba 2026, soko la fedha za kigeni baina ya mabenki liliendelea kuwa tulivu likichangiwa na uwepo wa ukwasi wa kutosha wa fedha za kigeni uliotokana na mauzo ya bidhaa nje ya nchi na shughuli za utalii. Sanjari na mwenendo huu, mauzo katika soko yalifikia dola za Marekani milioni 151.7, huku Benki Kuu ikiuza dola za Marekani milioni 7.2 kwa lengo la kupunguza athari za mabadiliko makubwa ya thamani ya shilingi katika soko (Kielelezo 2.4.3).

Kwa upande wa kiwango cha ubadilishaji fedha, shilingi ya Tanzania iliongezeka thamani kidogo, ikibadilishwa kwa wastani wa shilingi 2,654.91 kwa dola moja ya Marekani, ikilinganishwa na shilingi 2,657.01 mwezi Agosti 2026. Kwa ulinganifu wa mwaka kwa mwaka , thamani ya shilingi ilishuka thamani kwa asilimia 7.4, kwa kiasi kikubwa ikichangiwa na athari za mwaka wa kizio, kwani shilingi ilipanda thamani kwa kasi mwezi Septemba 2025.

Kielelezo 2.4.3: Mwenendo wa Soko la Fedhaza Kigeni



Chanzo: Benki Kuu ya Tanzani

Tanzania Yafungua Zaidi Milango ya Uwekezaji wa Mitaji Kimataifa.

Tarehe 17 Julai 2026, Kanuni za Fedha za Kigeni (Marekebisho) za mwaka 2026 zilichapishwa kupitia Tangazo la Serikali Na. 206 la mwaka 2026. Marekebisho haya yalibadilisha Kanuni ya 20 ya Kanuni za Fedha za Kigeni za mwaka 2022 kwa kuondoa vikwazo vya kijiografia pamoja na muda wa chini wa kumiliki dhamana. Hatua hii imefungua fursa kwa wawekezaji kutoka sehemu nyingine za dunia kuwekeza katika dhamana za Serikali ya Tanzania.

Ni muhimu kutambua kuwa Tanzania imekuwa ikifungua kwa hatua akaunti yake ya mitaji kwa wawekezaji wa kimataifa. Sheria ya Fedha za Kigeni ya mwaka 1992, Sheria ya Masoko ya Mitaji na Dhamana ya mwaka 1994, pamoja na kuanzishwa kwa Soko la Hisa la Dar es Salaam mwaka 1998, viliweka msingi wa maendeleo hayo.

Mwaka 2014, wakazi wa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki waliruhusiwa kushiriki kwa kiwango maalumu katika soko la dhamana za Serikali. Ruhusa hiyo iliwekewa ukomo wa asilimia 40 ya kila toleo la dhamana, pamoja na sharti la kutohamisha dhamana hizo kwenda kwa wakazi wa Tanzania ndani ya kipindi cha miezi 12. Mwaka 2022, kanuni mpya zilipanua fursa hiyo kwa wakazi wa nchi wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika na Watanzania wanaoishi nje ya nchi, huku muda wa chini wa kumiliki dhamana ukipunguzwa kutoka miezi 12 hadi miezi sita.

Marekebisho haya yanajengwa juu ya misingi imara ya uchumi jumla na maboresho ya hivi karibuni katika masoko

ya fedha. Mnada wa ushindani wa hati fungani za Serikali unaotumia Mfumo wa Kielektroniki wa Ulinganishaji wa Miamala (Electronic Matching System) ulianza kutumika Januari 2025. Mfumo wa kielektroniki wa fedha za kigeni kati ya benki ulianza kutumika Mei 2026, na mnyororo wa Viwango vya Riba vya Hatifungani za Serikali ya Tanzania (Tanzania Sovereign Yield Curve) ulizinduliwa mwezi Agosti 2026. Kwa hiyo, kupanua fursa za uwekezaji kutoka kwenye hati fungani za kampuni na hisa zilizoorodheshwa sokoni hadi kwenye dhamana za Serikali ni hatua ya kimantiki kuelekea kufungua zaidi akaunti ya mitaji na miamala ya kifedha kwa wawekezaji wa kimataifa.

Inatarajiwa kuwa kuongezeka kwa ushiriki wa wawekezaji wa kigeni kutachochea ushindani katika minada ya dhamana za Serikali. Hali hii inaweza kupunguza gharama za Serikali za kukopa na kusaidia utoaji wa dhamana zenye muda mrefu wa ukomavu. Vilevile, hatua hiyo inatarajiwa kuongeza ukwasi katika soko la pili la dhamana, kuboresha upatikanaji wa bei sahihi za dhamana, kuimarisha kielelezo cha faida rejea kinachotumika kama msingi wa upangaji wa bei za rasilimali fedha, na kuongeza ufanisi wa namna sera ya fedha inavyoathiri uchumi.

Aidha, uwekezaji wa wageni katika dhamana zinazotolewa kwa kutumia shilingi ya Tanzania unaweza kuongeza mapato ya fedha za kigeni nchini, kusaidia kuimarisha akiba ya fedha za kigeni na kuhamisha hatari ya mabadiliko ya kiwango cha ubadilishaji wa fedha kutoka kwa Serikali kwenda kwa wawekezaji.

Kwa muda mrefu, kuongezeka kwa kina na ukwasi katika soko la ndani la hati fungani kunaweza kuongeza uwezekano wa Tanzania kujumuishwa katika fahirisi za kimataifa za hati fungani. Hatua hii inaweza kupanua zaidi wigo wa wawekezaji na kurahisisha upatikanaji wa mitaji kutoka masoko ya kimataifa.

Hata hivyo, mageuzi haya yanaweza kuongeza uwezekano wa kukabiliwa na changamoto za mabadiliko ya viwango vya ubadilishaji wa fedha, kupungua kwa akiba ya fedha za kigeni na kupanda kwa viwango vya riba za dhamana iwapo wawekezaji watatoa mitaji yao kwa ghafla.

Pamoja na changamoto hizo, marekebisho ya Julai 2026 ni hatua muhimu kuelekea kuimarisha mtangamano wa masoko ya Tanzania na masoko ya fedha ya kimataifa. Manufaa ya mageuzi haya yanatarajiwa kuwa makubwa zaidi iwapo Tanzania itaendelea kudumisha misingi imara ya uchumi, ikiwemo mfumuko wa bei ulio chini na thabiti, nidhamu ya matumizi ya Serikali, akiba ya kutosha ya fedha za kigeni, pamoja na masoko ya fedha yenye uwazi na ufanisi.


2. 5 Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali

Ukusanyaji wa mapato ya Serikali ulikuwa wa kuridhisha mwanzoni mwa mwaka wa fedha 2026/27, ambapo mapato yaliyokusanywa yalifikia shilingi bilioni 3,502.2 mwezi Julai 2026, juu ya lengo kwa asilimia 9.5. Kati ya mapato hayo, Serikali Kuu ilichangia shilingi bilioni 3,354.9, ambayo ni sawa na asilimia 95.8 ya jumla ya mapato yaliyokusanywa.

Makusanyo ya kodi yaliendelea kuwa mazuri, yakifikia shilingi bilioni 2,877.0 sawa na asilimia 9.8 juu ya lengo la mwezi. Ufanisi huu ni matokeo ya maboresho yanayoendelea katika usimamizi wa kodi na ulipaji wa kodi kwa hiari. Kwa upande mwingine, mapato yasiyo ya kodi yalifikia shilingi bilioni 477.9, pungufu ya lengo la kukusanya shilingi bilioni 480.2 (Kielelezo 2.5.1).

Kielelezo 2.5.1: Mapato ya Serikali Kuu Mwezi Julai

Shilingi bilioni




Chanzo: Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: Takwimu halisi za mwaka 2026 ni za awali

Mwezi Julai 2026, Serikali iliendelea kuwianisha matumizi yake kuendana na mapato, ambapo ilitumia shilingi bilioni 3,572.4. Kati ya kiasi hicho shilingi bilioni 2,779.5 zilitumika kwa matumizi ya kawaida, huku shilingi bilioni 792.9 zilielekezwa kwenye miradi ya maendeleo (Kielelezo 2.5.2).

Kielelezo 2.5.2: Matumizi ya Serikali Kuu Mwezi Julai

Shilingi bilioni



Chanzo: Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: Takwimu halisi za mwaka 2026 ni za awali

2.6 Mwenendo wa Deni la Taifa

Deni la taifa (linalojumuisha deni la Serikali la ndani na la nje, na deni la nje la sekta binafsi) liliongezeka kidogo na kufikia dola za Marekani milioni 52,344.2 kutoka dola za Marekani milioni 52,341.1 mwishoni mwa mwezi uliotangulia. Deni la nje liliendelea kuchangia kiasi kikubwa cha deni lote, likifikia asilimia 70.3 (Kiambatisho, Jedwali A10).

Deni la Nje

Deni la nje, linalojumuisha deni la Serikali na sekta binafsi, liliongezeka kidogo ikilinganishwa na mwezi uliotangulia, na kufikia dola za Marekani milioni 36,784.2 mwishoni mwa mwezi wa mapitio. Katika kiasi hicho, asilimia 83.4 ilikuwa deni la nje la Serikali, huku sehemu iliyobaki ikiwa ni la sekta binafsi (Jedwali 2.6.1). Mikopo ya nje iliyopokelewa mwezi Septemba 2026 ilikuwa dola za Marekani milioni 234.3 ambapo sehemu kubwa ilipokelewa na Serikali Kuu. Aidha, kiasi cha dola za Marekani milioni 171.9 kilitumika kulipia deni la nje, ambapo dola za Marekani milioni 122 zilitumika kufanya malipo ya mkopo mkuu.

Mchanganuo wa deni la nje kwa aina ya wakopeshaji ulikuwa sawa na ule wa mwezi uliotangulia. Mashirika ya kifedha ya kimataifa yaliendelea kuwa wakopeshaji wakuu, yakichangia asilimia 59.5, yakifuatiwa na wakopeshaji wa kibiashara kwa asilimia 34.5 (Jedwali 2.6.2). Kwa mgawanyiko wa kisekta, mikopo kwa ajili ya urari wa malipo ya nje na bajeti iliendelea kuchukua sehemu kubwa ya mikopo yote, ikifuatiwa na mikopo kwa shughuli za usafirishaji na mawasiliano. Kwa mgawanyo wa sarafu, Dola ya Marekani iliendelea kuwa sarafu kuu ya deni la nje kwa asilimia 65.3, ikifuatiwa na sarafu ya Umoja wa Ulaya kwa asilimia 18.1 (Jedwali 2.6.3 na Jedwali 2.6.4).

Jedwali 2.6.1: Mchanganuo wa Deni la Nje Kwa Kundi la Wakopaji

Dola za Marekani Milioni

	Sep-25		Ago-26[r]		Sep-26[p]	
Mkopaji	Kiasi	Mchango (%)	Kiasi	Mchango (%)	Kiasi	Mchango (%)
Serikali Kuu	29,290.9	84.9	30,779.4	83.5	30,695.7	83.4
Deni ambalo halijalipwa	29,212.2	84.6	30,698.7	83.3	30,615.1	83.2
Malimbikizo ya riba	78.7	0.2	80.7	0.2	80.6	0.2
Sekta binafsi	5,218.5	15.1	6,068.8	16.5	6,088.5	16.6
Deni ambalo halijalipwa	5,115.0	14.8	5,838.1	15.8	5,839.2	15.9
Malimbikizo ya riba	103.6	0.3	230.6	0.6	249.3	0.7
Mashirika ya umma	0.6	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0
Deni ambalo halijalipwa	0.6	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0
Malimbikizo ya riba	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0
Jumla ya deni la nje	34,510.1	100.0	36,848.2	100.0	36,784.2	100.0

Chanzo: Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: r, inamaanisha takwimu zilizorekebishwa; p, takwimu za awali; na TANESCO, ATCL, TRC, TPA, TFC na DAWASA hazina deni la nje ambalo halijalipwa

Jedwali 2.6.2: Mchanganuo wa Deni la Nje kwa Kundi la Wakopeshaji

Dola za Marekani Milioni

	Sep-25		Aug-26[r]		Sep-26[p]	
Mkopeshaji	Kiasi	Mchango (%)	Kiasi	Mchango (%)	Kiasi	Mchango (%)
Mashirika ya fedha ya kimataifa	20,230.1	58.6	21,899.2	59.4	21,892.2	59.5
Deni ambalo halijalipwa	20,208.0	58.6	21,874.6	59.4	21,867.5	59.4
Malimbikizo ya riba	22.1	0.1	24.7	0.1	24.7	0.1
Nchi washirika wa maendeleo	1,559.3	4.5	1,561.1	4.2	1,547.4	4.2
Deni ambalo halijalipwa	1,480.6	4.3	1,480.4	4.0	1,466.8	4.0
Malimbikizo ya riba	78.7	0.2	80.7	0.2	80.6	0.2
Benki za kimataifa za biashara	12,042.8	34.9	12,721.4	34.5	12,677.7	34.5
Deni ambalo halijalipwa	11,984.0	34.7	12,555.4	34.1	12,495.1	34.0
Malimbikizo ya riba	58.9	0.2	166.0	0.5	182.6	0.5
Mikopo ya mauzo ya nje	677.8	2.0	666.4	1.8	666.9	1.8
Deni ambalo halijalipwa	655.2	1.9	626.4	1.7	624.9	1.7
Malimbikizo ya riba	22.6	0.1	40.0	0.1	42.0	0.1
Jumla ya deni la nje	34,510.1	100.0	36,848.2	100.0	36,784.2	100.0

Chanzo: Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: r, inamaanisha takwimu zilizorekebishwa; na p, takwimu za awali

Jedwali 2.6.3: Mchanganuo wa Deni la Nje kwa Aina ya Matumizi.

Asilimia

Shughuli ya uchumi	Sep-25	Ago-26[r]	Sep-26[p]
Urari wa malipo yote ya nje, na bajeti (BOP and budget support)	23.2	23.5	23.2
Usafirishaji na mawasiliano	21.7	20.8	21.0
Kilimo	5.0	5.5	5.5
Nishati na madini	11.8	12.7	12.8
Viwanda	2.9	3.4	3.5
Huduma za jamii na elimu	19.7	19.3	19.3
Fedha na bima	3.5	4.2	4.2
Utalii	1.8	1.6	1.6
Mali isiyohamishika na ujenzi	5.4	4.8	4.8
Mengineyo	5.1	4.2	4.2
Jumla	100.0	100.0	100.0

Chanzo: Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: r, inamaanisha takwimu zilizorekebishwa; na p, takwimu za awali

Jedwali 2.6.4: Mchanganuo wa Deni la Nje kwa Aina ya Sarafu.

Asilimia

Sarafu	Sep-25	Ago-26[r]	Sep-26[p]
Dola ya Marekani	65.9	65.0	65.3
Sarafu ya umoja wa Ulaya (Euro)	17.7	18.3	18.1
Yuan ya China	6.5	6.7	6.7
Sarafu nyinginezo	9.9	9.9	10.0
Jumla	100.0	100.0	100.0


Chanzo: Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: r, inamaanisha takwimu zilizobadilishwa; na p, takwimu za awali

Deni la Ndani

Deni la ndani la Serikali, lilifikia shilingi bilioni 41,113.5 mwishoni mwa mwezi Septemba 2026, likiongezeka kidogo kutoka kiwango kilichorekodiwa mwezi uliotangulia (Kielelezo 2.6.1 na Jedwali 2.6.5). Benki za biashara na mifuko ya hifadhi ya jamii iliendelea kuwa wakopeshaji wakubwa wa Serikali, kwa pamoja ikikopesha zaidi ya nusu ya jumla ya deni la Serikali (Jedwali 2.6.6).

Kielelezo 2.6.1: Deni la Ndani la Serikali Kuu

Shilingi Bilioni



Chanzo: Wizara ya Fedha

Jedwali 2.6.5: Deni la Ndani la Serikali kuu kwa Vyanzo vya Mikopo

Shilingi Bilioni

	Sep-25		Ago-26		Sep-26[P]	
Nyenzo	Kiasi	Mchango (%)	Kiasi	Mchango (%)	Kiasi	Mchango (%)
Dhamana za serikali	32,498.5	86.8	36,722.5	89.8	36,827.7	89.6
Dhamana za serikali za muda mfupi	2,058.7	5.5	1,793.4	4.4	1,896.4	4.6
Hisa za serikali	135.8	0.4	135.7	0.3	135.7	0.3
Dhamana za serikali za muda mrefu	30,304.0	80.9	34,793.4	85.1	34,795.6	84.6
Vyeti vya ushuru	0.1	0.0	0.1	0.0	0.1	0.0
Deni lisilo na dhamana	4,960.5	13.2	4,176.9	10.2	4,285.8	10.4
Madeni mengine*	18.4	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0
Bakaa hasi	4,942.1	13.2	4,176.9	10.2	4,285.8	10.4
Deni la ndani (ukiondoa karatasi za ukwasi)	37,459.0	100.0	40,899.5	100.0	41,113.5	100.0

Chanzo: Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: p, inamaanisha takwimu za awali; na madeni mengine yanajum uisha mkopo wa biashara na marejesho ya kodi ya ushuru

Jedwali 2.6.6: Deni la Ndani la Serikali Kuu kwa Kundi la Wakopeshaji

Shilingi Bilioni

	Sep-25		Ago-26		Sep-26[P]	
Mkopeshaji	Kiasi	Mchango (%)	Kiasi	Mchango (%)	Kiasi	Mchango (%)
Benki za biashara	10,752.0	28.7	11,599.3	28.4	11,703.1	28.5
Benki Kuu ya Tanzania	6,750.9	18.0	7,054.9	17.2	7,163.8	17.4
Mifuko ya hifadhi ya jamii	10,282.0	27.4	11,292.5	27.6	11,256.1	27.4
Kampuni za bima	1,825.1	4.9	2,050.4	5.0	2,030.1	4.9
Mifuko maalumu ya Benki Kuu	780.5	2.1	867.6	2.1	865.1	2.1
Wengine	7,068.6	18.9	8,034.7	19.6	8,095.4	19.7
Deni la ndani (ukiondoa karatasi za ukwasi)	37,459.0	100.0	40,899.5	100.0	41,113.5	100.0


Chanzo: Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: p, inamaanisha takwimu za awali; na “wengine” inajumuisha taasisi za umma, kampuni, watu binafsi, na wawekezaji wasio wakazi.

Ili kufadhili bajeti, Serikali ilikopa jumla ya shilingi bilioni 356 kutoka soko la ndani kupitia dhamana za Serikali mwezi Septemba 2026. Kiasi hicho kilijumuisha shilingi bilioni 178 zilizopatikana kupitia uuzaji wa hati fungani za Serikali na shilingi bilioni 178 kupitia dhamana za Serikali za muda mfupi za siku 364 (Kielelezo 2.6.2). Wakati

huohuo, malipo ya deni la ndani yalifikia jumla ya shilingi bilioni 556.4, yakijumuisha marejesho ya deni la msingi ya shilingi bilioni 250.8 na malipo ya riba ya shilingi bilioni 305.6.

Kielelezo 2.6.2: Dhamana za Serikali Zilizotolewa kwa Madhumuni ya Ufadhili wa Bajeti

Shilingi Bilioni



Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

2.7 Mwenendo wa Sekta ya Nje

Sekta ya nje iliendelea kukabiliwa na athari kubwa zilizotokana na migogoro inayoendelea Mashariki ya Kati. Hali hiyo ilisababisha kuongezeka kwa nakisi ya urari wa malipo ya kawaida hadi dola za Marekani milioni 2,397.5 mwaka ulioishia Septemba 2026, kutoka dola za Marekani milioni 1,879.3 katika kipindi kama hicho mwaka 2025 (Jedwali 2.7.1). Kuongezeka kwa nakisi kuaashiria ukuaji zaidi wa uagizaji wa bidhaa na huduma ikilinganishwa na ukuaji wa mauzo ya bidhaa na huduma. Hata hivyo, mapato yatokanayo na mauzo ya bidhaa na huduma yalifidia kwa kiasi kudorora kwa nakisi ya urari wa malipo.

Akiba ya fedha za kigeni ilifikia dola za Marekani milioni 6,031.9 mwishoni mwa Septemba 2026, kiasi kinachotosheleza kugharamia uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi cha miezi 4.3, ikiwa ni juu ya lengo la kitaifa. Utoshelevu huu ulichangiwa na mapato yatokanayo na mauzo ya bidhaa na huduma pamoja na mpango wa Benki Kuu wa ununuzi wa dhahabu (Kielelezo 2.7.1).

Jedwali 2.7.1 Urari wa Biashara ya Bidhaa, Huduma na Uhamisho Mali


Dola za Marekani Milioni

				Mwaka ulioishia Septemba			Mabadiliko
	Sep-25	Ago-26	Sep-26	2024	2025	2026^{p}	ya asilimia
Urari wa bidhaa	-573.8	-888.2	-318.5	-5,928.7	-4,596.3	-6,241.2	35.8
Zilozouzwa nje*	1013.1	1,196.6	1,504.1	8,226.5	10,060.1	12,444.9	23.7
Zilizonunuliwa nje	1,586.9	2,084.7	1,822.6	14,155.2	14,656.4	18,686.1	27.5
Urari wa huduma	432.96	696.8	729.3	4,062.9	4,315.9	5,172.2	19.8
Mapato	703.5	989.1	1,017.5	6,667.1	7,508.3	8,620.2	14.8
Malipo	270.6	292.3	288.2	2,604.2	3,192.4	3,448.1	8.0
Urari wa bidhaa na huduma	-140.8	-191.4	410.8	-1,865.8	-280.4	-1,069.0	281.3
Bidhaa na huduma zilizouzwa nje	1,716.6	2,185.6	2,521.6	14,893.6	17,568.5	21,065.1	19.9
Bidhaa na huduma zilizonunuliwa kutoka nje	1,857.4	2,377.0	2,110.8	16,759.4	17,848.9	22,134.2	24.0
Urari wa malipo wa vitega uchumi	-137.6	-115.5	-123.0	-1,735.4	-2,073.6	-2,089.8	0.8
Yaliyoingia	52.3	18.5	20.5	321.7	328.8	241.1	-26.7
Yaliyotoka	190.0	134.0	143.6	2,057.1	2,402.3	2,330.9	-3.0
Urari wa uhamisho mali ya kawaida	26.0	108.7	133.4	585.2	474.6	761.4	60.4
Iliyoingia	98.3	140.2	161.6	1,263.5	1,080.3	1,309.8	21.2
ambapo Serikali	1.4	0.0	0.0	127.9	99.0	35.3	-64.4
Iliyotoka	72.3	31.5	28.2	678.4	605.7	548.5	-9.4
Urari wa Bidhaa, Huduma na Uhamisho Mali	-252.5	-198.2	421.2	-3,016.0	-1,879.3	-2,397.5	27.6

Chanzo: Mamlaka ya Mapato Tanzania na Benki Kuu ya Tanzania

Tanbihi: p, inamaanisha takwimu za awali na *zinajumuisha marekebisho ya mauzo nje ya nchi ambayo hayajarekodiwa kikamilifu

Kielelezo 2.7.1 Akiba ya Fedha za Kigeni



Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

Mauzo ya nje


Mauzo ya nje ya bidhaa na huduma yaliongezeka kwa asilimia 19.9 hadi kufikia dola za Marekani milioni 21,065.1 katika mwaka ulioishia Septemba 2026, kutoka dola za Marekani milioni 17,568.9 katika kipindi kama hicho mwaka 2025. Ongezeko hilo lilitokana na kuimarika kwa mauzo ya dhahabu, mapato yatokanayo na huduma za utalii, bidhaa za viwandani na bidhaa asilia. Mauzo ya bidhaa nje ya nchi yaliongezeka kwa asilimia 23.7 hadi dola za Marekani milioni 12,444.9, kutoka dola za Marekani milioni 10,060.1 katika kipindi kama hicho mwaka 2025. Ukuaji huo ulichangiwa zaidi na mauzo ya dhahabu na bidhaa za viwandani (Kielelezo 2.7.2). Mauzo ya dhahabu yaliongezeka hadi dola za Marekani milioni 5,834.9 kutoka dola za

Marekani milioni 4,431.2, kutokana na bei nzuri katika soko la dunia pamoja na uzalishaji wa ndani. Vilevile, mauzo ya bidhaa za viwandani yaliongezeka hadi dola za Marekani milioni 2,202.4 kutoka dola za Marekani milioni 1,546.2, yakichangiwa na ongezeko la mauzo ya bidhaa za chuma na vioo.

Mauzo ya mazao ya bidhaa asilia yaliongezeka, yakichangiwa zaidi na mauzo ya tumbaku, hata hivyo, mauzo ya kahawa na korosho yalipungua, licha ya kuendelea kuwa miongoni mwa mazao muhimu ya biashara yanayouzwa nje ya nchi. Kwa ulinganifu wa mwezi kwa mwezi, mauzo ya bidhaa nje ya nchi yaliongezeka hadi dola za Marekani milioni 1,504.1 Septemba 2026, ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 1,013.1 Septemba 2025, ikichangiwa zaidi na mauzo ya dhahabu.

Kielelezo 2.7.2: Mauzo ya Nje ya Bidhaa na Huduma

Dola za Marekani Milioni




Chanzo: Mamlaka ya Mapato Tanzania na Uchambuzi wa Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: p, inamaanisha takwimu za awali

Mapato yatokanayo na huduma yaliongezeka kwa asilimia 14.8 hadi dola za Marekani milioni 8,620.2 katika mwaka ulioishia Septemba 2026, kutoka dola za Marekani milioni 7,508.8 katika kipindi kama hicho mwaka 2025. Ongezeko hilo lilitokana zaidi na kuongezeka kwa mapato yatokanayo na utalii na huduma za usafirishaji. Mapato ya utalii yaliongezeka hadi dola za Marekani milioni 4,565.8 kutoka dola za Marekani milioni 4,387.6, ikiakisi kuendelea kukua kwa shughuli za utalii (Kielelezo 2.7.3).

Mapato yatokanayo na huduma za usafirishaji yaliongezeka kwa kiasi kikubwa hadi dola za Marekani milioni 3,478.7 kutoka dola za Marekani milioni 2,669.9, yakichangiwa na ongezeko la mapato ya huduma za usafirishaji wa mizigo kwenda nchi jirani. Kwa ulinganifu wa mwezi kwa mwezi, mapato yatokanayo na huduma yalifikia dola za Marekani milioni 1,017.5 Septemba 2026, kutoka dola za Marekani milioni 703.7 Septemba 2025, yakichangiwa zaidi na mapato ya utalii.

Kielelezo 2.7.3: Mapato ya Huduma kwa Sekta

Dola za Marekani Milioni



Chanzo: Uchambuzi wa Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: Huduma nyinginezo zinajumuisha ujenzi, bima,huduma za fedha, mawasiliano ya simu, komputa na taarifa, ada za matumizi ya mali miliki ya kiakili, huduma za serikali, huduma binafsi, na huduma nyingine za kibiashara.

Uagizaji wa Bidhaa na Huduma


Uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje uliongezeka kwa asilimia 24 hadi dola za Marekani milioni 22,134.2 mwaka ulioishia Septemba 2026, kutoka dola za Marekani milioni 17,848.9 kipindi kama hicho mwaka 2025. Ongezeko kubwa lilionekana katika uagizaji wa bidhaa za viwandani, bidhaa za petroli, malipo ya huduma za usafirishaji wa mizigo, na vifaa vya usafirishaji viwandani. Ongezeko la uagizaji wa bidhaa za

kati na bidhaa mtaji linaashiria kuimarika kwa uwekezaji wa sekta ya umma na binafsi pamoja na ukuaji wa shughuli za viwanda. Uagizaji wa bidhaa za petroli, zilizochangia takribani asilimia 20 ya jumla ya uagizaji wa bidhaa kutoka nje, uliongezeka kwa asilimia 72.3 hadi dola za Marekani milioni 3,813.6 kutokana na kupanda kwa bei katika soko la dunia kufuatia mgogoro unaoendelea Mashariki ya Kati (Kielelezo 2.7.4).

Kwa ulinganifu wa mwezi kwa mwezi, uagizaji wa bidhaa kutoka nje ulifikia dola za Marekani milioni 1,822.6 mwezi Septemba 2026, ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 1,586.9 mwezi Septemba 2025.

Kielelezo 2.7.4: Ulinganifu wa Uagizaji wa Bidhaa na Huduma

Dola za Marekani Milioni




Chanzo: Mamlaka ya Mapato Tanzania na Uchambuzi wa Benki Kuu ya Tanzania

Tanbihi: p, inamaanisha takwimu za awali.

Malipo ya huduma yaliongezeka kwa asilimia 8 hadi dola za Marekani milioni 3,448.1 mwaka ulioishia Septemba 2026, kutoka dola za Marekani milioni 3,192.4 kipindi kama hicho mwaka 2025. Ongezeko hilo lilichangiwa zaidi na kuongezeka kwa malipo ya usafirishaji wa mizigo, sawia na ongezeko la gharama za uagizaji wa bidhaa kutoka nje (Kielelezo 2.7.5).

Kwa ulinganifu wa mwezi kwa mwezi, malipo ya huduma yalifikia dola za Marekani milioni 288.2 mwezi Septemba 2026, kutoka dola za Marekani milioni 270.6 mwezi Septemba 2025, yakichangiwa zaidi na malipo ya usafirishaji wa mizigo.

Kielelezo 2.7.5: Malipo ya Huduma Dola za Marekani Milioni



Chanzo: Uchambuzi wa Benki kuu ya Tanzania

Tanbihi: Huduma nyingine zinajumuisha ujenzi, bima, huduma za kifedha, mawasiliano ya simu, kompyuta na taarifa, ada za matumizi ya mali miliki ya kiakili,huduma za kiserikali,huduma binafsi, na huduma nyingine za kibiashara.

Katika mwaka ulioishia Septemba 2026, nakisi ya urari wa mapato ya vitega uchumi iliongezeka hadi dola za Marekani milioni 2,089.8, kutoka dola za Marekani milioni 2,073.6 kipindi kama hicho mwaka 2025. Hali hiyo ilitokana zaidi na kuongezeka kwa malipo ya nje. Kwa ulinganifu wa mwezi kwa mwezi, nakisi ya urari wa mapato ya vitega uchumi ilipungua hadi dola za Marekani milioni 123 Septemba 2026, ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 137.6 Septemba 2025.

Ziada ya urari wa uhamisho wa mali wa kawaida iliongezeka hadi dola za Marekani milioni 761.4 mwaka ulioishia Septemba 2026, kutoka dola za Marekani milioni 474.6 kipindi kama hicho mwaka 2025. Ongezeko hilo lilichangiwa zaidi na uhamisho binafsi wa fedha. Kwa ulinganifu wa mwezi kwa mwezi, ziada ya urari wa uhamisho wa mali wa kawaida iliongezeka hadi dola za Marekani milioni 133.4 Septemba 2026, kutoka dola za Marekani milioni 26 Septemba 2025.

3.0 Mwenendo wa Uchumi wa Zanzibar

3.1 Mfumuko wa Bei

Mfumuko wa bei ulikuwa ndani ya lengo la muda wa kati wa asilimia 3 hadi 5. Mfumuko wa bei wa jumla ulipungua hadi asilimia 4.3 mwezi Septemba 2026, ikilinganishwa na asilimia 5.6 ya mwezi uliotangulia. Kupungua huko, kulisababishwa na kushuka kwa bei za vyakula na vinywaji visivyo na kilevi, ambavyo vina uzito wa asilimia 41.9 katika kapu la fahirisi za bei. Hata hivyo, mfumuko wa bei ulikuwa juu ya asilimia 3.5 iliyorekodiwa kipindi kama hicho mwaka 2025 (Jedwali 3.1.1). Kwa ulinganifu wa mwezi kwa mwezi, mfumuko wa bei wa jumla ulikiwa asilimia -1 mwezi Septemba 2026, ikilinganishwa na asilimia - 0.2 iliyorekodiwa mwezi Septemba 2025.

Jedwali 3.1.1: Mwenendo wa Mfumuko wa Bei


Asilimia (Kizio: Julai 2022 =100)

Kundi	Uzito	Mabadiliko kila Mwezi			Mabadiliko kila Mwaka		
		Sep-25	Ago-26	Sep-26	Sep-25	Ago-26	Sep-26
Vyakula na Vinywaji Visivyo na Kileo	41.9	0.7	-0.4	-1.9	4.7	9.6	6.8
Vinywaji vyenye Vileo, Tumbaku na Madawa ya binadamu	0.2	0.0	0.1	0.0	2.7	4.2	4.2
Mavazi na Viatu	6.3	0.0	0.1	0.0	5.6	1.5	1.5
Makazi, Maji, Umeme, Gesi na Nishati Nyingine	25.8	-0.6	-0.5	-0.3	1.1	1.0	1.3
Samani, Vifaa vya Nyumbani na Matengenezo ya Kawaida ya Nyumba	4.8	0.0	0.0	0.5	3.7	4.3	4.8
Afya	1.3	0.0	0.0	0.0	1.6	0.9	0.9
Uchukuzi	9.1	0.4	0.3	0.0	2.2	5.2	4.7
Taarifa na mawasiliano	4.2	0.0	0.0	0.0	2.7	0.3	0.3
Burudani, Michezo na Utamaduni	1.1	1.9	0.4	0.0	6.2	3.0	1.2
Elimu	1.6	0.0	0.8	0.0	3.8	1.1	1.1
Huduma za Migahawa na Malazi	1.4	0.0	0.0	0.0	1.6	6.2	6.2
Bima na Huduma za Fedha	0.5	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0
Huduma binafsi, Ulinzi wa Kijamii na Bidhaa na Huduma Mbalimbali	1.7	0.4	0.0	0.1	5.8	1.1	0.8
Mfumuko wa bei wa jumla	100.0	0.2	-0.2	-1.0	3.5	5.6	4.3
Mfumuko wa bei wa bidhaa za chakula	40.5	0.7	-0.4	-2.0	4.1	9.8	6.9
Mfumuko wa bei wa bidhaa zisizo za chakula	59.5	-0.2	-0.1	-0.1	2.9	2.2	2.3

Chanzo: Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Zanzibar


Kielelezo 3.1.1: Mfumuko wa Bei wa Mwaka

Asilimia



Chanzo: Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Zanzibar

Kielelezo 3.1.2: Wastani wa Bei za Rejareja za Mafuta ya Petroli kwa Mwezi




Chanzo: Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Zanzibar

3.2 Bajeti ya Serikali

Mwezi Septemba 2026, mapato ya Serikali yalifikia shilingi bilioni 210.4, sawa na asilimia 92.8 ya lengo la mwezi. Mapato ya ndani yalifikia shilingi bilioni 200.9, ikiwa ni asilimia 95.5 ya mapato yote, na asilimia 92.9 ya lengo la mwezi, huku kiasi kilichobaki kikiwa ni misaada. Mapato ya kodi, yaliendelea kuwa chanzo kikuu cha mapato ya ndani yakichangia asilimia 86.4 ya makusanyo yote na kufikia kiasi cha shilingi bilioni 173.7, sawa na asilimia 91.6 ya lengo. Mwenendo huu ulichangiwa na makusanyo ya kuridhisha ya kodi ya ongezeko la thamani, ushuru wa bidhaa za ndani na kodi ya mapato. Mapato yasiyo ya kodi yalifikia shilingi bilioni 27.3, yakizidi lengo la mwezi kwa asilimia 2.4, yakiakisi kuimarika kwa ukusanyaji wa mapato katika taasisi za Serikali (Kielelezo 3.2.1).

Kielelezo 3.2.1: Mapato ya Serikali

Shilingi Bilioni




Chanzo: Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango, Zanzibar

Tanbihi: Kodi nyingine zinahusisha tozo za hoteli, tozo za wasindikiza wageni, stampu za tozo, tozo za huduma za viwanja vya ndege na bandari, tozo za maendeleo ya barabara na petroli

Matumizi ya Serikali yalikuwa shilingi bilioni 494.4 katika mwezi wa mapitio, kulingana na rasilimali zilizopo. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 355.9 zilielekezwa katika matumizi ya maendeleo. Asilimia 77.8 ya matumizi yote katika miradi ya maendeleo, zilitokana na vyanzo vya ndani. Asilimia 28 ya matumizi yote yaliyobaki yalielekezwa katika matumizi ya kawaida (Kielelezo 3.2.2).

Kielelezo 3.2.2: Matumizi ya Serikali

Shilingi Bilioni



Chanzo:Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango, Zanzibar

Tanbihi: Matumizi mengine yanahusisha uhamisho wa fedha, malipo ya riba ya deni la ndani, huduma za mfuko mkuu wa serikali na tozo zingine

3.3 Mwenendo wa Sekta ya Nje

Katika mwaka ulioishia Septemba 2026, urari wa malipo ya kawaida uliimarika huku ziada ikiongezeka kwa asilimia 4.2 na kufikia dola za Marekani milioni 986.8, ikilinganishwa na kiwango kilichorekodiwa katika kipindi kama hicho mwaka uliotangulia. Matokeo hayo yalitokana na kuongezeka kwa mapato yatokanayo na huduma, hususan shughuli zinazohusiana na utalii (Jedwali 3.3.1).

Jedwali 3.3.1: Urari wa Malipo

Dola za Marekani Milioni

Maelezo	Sep-25	Ago-26	Sep-26	Mwaka unaoishia Septemba 2025	Mwaka unaoishia Septemba 2026[p]	Ongezeko/ Upungufu (Asilimia)
Urari wa bidhaa (Halisi)	-51.3	-56.6	-49.5	-532.2	-768.5	44.4
Zilizouzwa nje	6.1	1.9	1.9	35.2	65.0	84.9
zilizonunuliwa kutoka nje	57.4	58.5	51.4	567.4	833.5	46.9
Urari wa huduma (halisi)	143.4	221.4	169.7	1,470.1	1,733.6	17.9
Mapato	153.0	226.3	174.7	1,573.8	1,799.4	14.3
Malipo	9.7	5.0	5.0	103.7	65.9	-36.5
Urari wa bidhaa na huduma (halisi)	92.1	164.7	120.2	937.9	965.1	2.9
Bidhaa na huduma zilizouzwa nje	159.1	228.2	176.6	1,609.0	1,864.4	15.9
Bidhaa na huduma zilizonunuliwa kutoka nje	67.0	63.5	56.4	671.1	899.4	34.0
Urari wa mapato ya msingi (halisi)	0.5	2.6	3.0	8.2	17.1	---
Yaliyoingia	0.7	2.7	3.2	11.4	19.0	65.8
Yaliyotoka	0.2	0.1	0.2	3.3	1.8	-44.1
Urari wa uhamishaji Mali (halisi)	0.0	0.9	1.1	0.8	4.6	---
Iliyoingia	0.0	0.9	1.2	1.8	5.3	---
Iliyotoka	0.0	0.0	0.0	1.0	0.7	-34.6
Urari wa Bidhaa,huduma na uhamishaji mali	92.6	168.2	124.4	946.8	986.8	4.2

Chanzo: Mamlaka ya Mapato Tanzania, benki na uchambuzi wa Benki Kuu ya Tanzania

Tanbihi: p, inaashiria Takwimu za awali; fob, 'Mzigo ndani ya chombo

Mauzo ya nje

Thamani ya mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi iliongezeka kwa asilimia 15.9 hadi kufikia dola za Marekani milioni 1,864.4 mwaka ulioishia Septemba 2026, kutoka kiwango kilichorekodiwa kipindi kama hicho mwaka 2025 (Jedwali 3.3.1). Ongezeko hilo kwa kiasi kikubwa lilitokana na mapato zaidi yatokanayo na huduma, hususan shughuli zinazohusiana na utalii, pamoja na kuongezeka kwa uzalishaji na mauzo ya karafuu nje ya nchi. Mauzo ya karafuu yaliongezeka kwa kiasi kikubwa kufikia dola za Marekani milioni 38 mwaka ulioishia Septemba 2026, kutoka dola za Marekani milioni 6.2 katika kipindi kama hicho mwaka 2025, kutokana na mzunguko wa asili wa uzalishaji wa zao hilo (Jedwali 3.3.2).

Kwa ulinganifu wa mwezi kwa mwezi, mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi yaliongezeka na kufikia dola za Marekani milioni 176.6, kutoka dola za Marekani milioni 159.1 zilizorekodiwa mwezi Septemba 2025.

Jedwali 3.3.2: Uuzaji wa Bidhaa

Dola za Marekani Milioni

Maelezo	Uniti	Sep-25	Ago-26	Sep-26	Mwaka unaoishia Septemba 2025	Mwaka unaoishia Septemba 2026[p]	Ongezeko/Upungufu (Asilimia)
Mauzo ya nje ya bidhaa za asili							
Karafuu							
Thamani	000' ya USD	4,732.5	216.2	218.3	6,212.1	37,980.4	---
Kiasi	000' kwa Tani	0.7	0.1	0.1	1.1	6.5	
Bei kwa Unit	USD/Tani	6,802.4	3,891.4	3,969.6	4,009.3	4,049.4	
Mauzo ya nje ya bidhaa zisizo za asili Mwani							
Thamani	000' ya USD	88.2	135.0	136.4	2,959.0	1,359.5	-54.1
Kiasi	000' kwa Tani	0.2	0.2	0.2	5.4	2.2	
Bei kwa Unit	USD/Tani	550.5	647.9	660.9	667.6	674.2	
Bidhaa za Viwandani	000' ya USD	1,223.9	1,143.7	1,155.2	18,010.7	11,505.9	-36.1
Bidhaa za samaki	000' ya USD	30.0	49.3	49.8	658.5	1,072.2	62.8
Mauzo ya nje ya nchini kwa bidhaa nyingine	000' ya USD	26.8	330.6	333.9	7,310.9	13,064.0	78.7
Jumla Ndogo	000' ya USD	1,368.9	1,658.6	1,675.2	28,939.0	27,001.7	-6.7
Jumla Kuu	USD ('000')	6,101.5	1,874.8	1,893.6	35,151.1	64,982.0	84.9

Chanzo: Mamlaka ya Mapato Tanzania na uchambuzi wa Benki Kuu ya Tanzania

Uagizaji wa bidhaa na huduma

Uagizaji wa bidhaa na huduma uliongezeka kwa asilimia 34 nakufikia dola za Marekani milioni 899.4 mwaka ulioishia Septemba 2026, ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka 2025 (Jedwali 3.3.1). Ongezeko hilo lilichangiwa zaidi na uagizaji wa bidhaa za mtaji, hususan mashine na mitambo. Vilevile uagizaji wa bidhaa za matumizi uliongezeka, hasa vyakula na vinywaji (Jedwali 3.3.3).

Kwa ulinganifu wa mwezi kwa mwezi, uagizaji wa bidhaa na huduma ulifikia dola za Marekani milioni 56.4 mwezi Septemba 2026, ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 67 zilizorekodiwa katika mwezi kama huo mwaka 2025.

Jedwali 3.3.3: Uagizaji wa Bidhaa

Dola za Marekani Milioni

Maelezo	Sep-25	Ago-26	Sep-26	Mwaka unaoishia Septemba 2025	Mwaka unaoishia Septemba 2026[p]	Ongezeko/Upungufu (Asilimia)
Bidhaa za Mtaji	13.2	16.7	16.9	81.2	228.3	---
Mitambo na vifaa vya kimitambo	4.3	7.0	7.1	30.6	84.2	---
Vifaa vya usafirishaji Kiwandani	2.7	5.0	5.0	25.2	78.6	---
Mashine na Vifaa vya Umeme	4.3	3.2	3.2	16.6	48.2	---
Bidhaa nyingine za mtaji	2.0	1.5	1.0	8.8	16.4	85.7
Bidhaa za uzalishaji wa kati	33.1	34.2	26.8	409.6	494.2	20.7
Vifaa vya viwandani	19.2	24.5	24.7	148.1	254.7	72.0
Ambazo ni chuma na bidhaa zinazotokana navyo	6.1	11.4	11.5	28.3	81.5	---
Plastiki na bidhaa zake	1.7	2.8	2.8	9.2	22.4	---
Nishati na mafuta	1.0	0.3	0.3	134.3	120.1	-10.5
ambazo ni bidhaa safi za mafuta	1.0	0.2	0.2	134.2	115.4	-14.0
Vifaa	3.8	6.7	6.8	19.7	54.9	---
Chakula na Vinywaji kwa Matumizi ya Viwandani	7.4	1.8	1.8	86.6	54.2	-37.4
Ambazo ni nafaka ya ngano	3.3	0.0	0.0	27.0	18.3	-32.3
Mafuta ya kula	3.9	0.7	0.7	41.0	17.2	-58.1
Magari ya matumizi ya nyumbani	1.5	0.9	0.9	20.9	18.0	-13.8
Bidhaa za Matumizi ya Mwisho	11.0	7.6	7.7	76.5	111.0	45.0
Chakula na vinywaji vinavyotumika hasa kwa matumizi ya nyumbani	1.3	1.4	1.4	16.5	19.7	19.8
Vifaa vya Usafirishaji Visivyo vya Viwandani	0.3	0.5	0.5	2.5	4.4	75.9
Ambazo ni pikipiki na baiskeli zilizowekwa na mota ndogo ya ziada	0.1	0.2	0.2	1.0	1.7	65.3
Bidhaa nyingine za matumizi ya mwisho	9.4	5.8	5.8	57.5	83.2	44.7
Ambazo ni bidhaa za dawa	0.0	0.1	0.2	4.4	1.6	-64.3
Saburi na dawa za kusafisha	0.7	0.7	0.7	5.0	8.1	60.4
Vitambaa na Mavazi	0.8	0.6	0.6	5.7	8.2	44.2
Viatu na bidhaa nyingine	0.4	0.3	0.3	3.2	4.1	31.0
Karatasi na bidhaa zake	0.1	0.0	0.0	2.0	1.3	-31.9
Jumla (f.o.b)	57.4	58.5	51.4	567.4	833.5	46.9

Chanzo: Mamlaka ya Mapato Tanzania na uchambuzi wa Benki Kuu ya Tanzania

Tanbihi: p inaashiria takwimu za awali; "---", badiliko linalozidi asilimia 100; f.o.b mzigo ndani ya chombo

VIAMBATISHO

Jedwali A1: Viashiria vya Kiuchumi

		2018	2019	2020	2021	2022	2023	2024[r]	2025[p]
Ukuaji wa Pato la Taifa na Mfumuko wa bei									
1. 1Ukuaji wa Pato la Taifa kwa Bei za Miaka Husika	Asilimia	4.4	8.5	8.1	7.4	9.4	10.5	10.2	na
1.2 Ukuaji halisi wa Pato ta Taifa	Asilimia	7.0	6.9		4.8	4.7	5.1	5.5	6.0
1.3 Wastani Pato kwa Kila Mtu kwa bei za miaka inayohusika	'000' sh	2,356.5	2,479.3	2,597.7	2,705.4	2,854.1	3,058.8	3,234.9	na
1.4 Wastani Pato kwa Kila Mtu kwa bei za miaka inayohusika	Dola ya Marekani	1,041.0	1,083.5	1,126.7	1,171.6	1,233.1	1,263.1	1,239.2	na
1.5 Kasi ya Upandaji wa Bei	Asilimia	3.5	3.4	3.3	3.7	4.3	3.8	3.1	3.3
1.6 Uwiano wa Akiba kwa Pato halisi la Taifa	Asilimia	18.7	18.6	16.5	17.3	19.7	21.2	25.8	na
Takwimu za Kifedha na Riba									
2.1 Ukuaji wa Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3)	Asilimia	4.5	9.6	5.7	15.5	11.6	14.1	11.1	24.7
2.2.Ukuaji wa Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana (M2)	Asilimia	3.8	11.8	8.2	17.6	12.1	11.9	9.2	28.5
2.3 Ukuaji va Ujazi wa fedha, kwa tafsiri finyu (M1)	Asilimia	5.1	13.7	7.5	23.1	7.5	8.7	11.2	30.2
2.4 Ukuaji Fedha ya msingi (M0)	Asilimia	0.6	6.8	-4.0	17.3	15.8	3.7	19.1	20.7
2.5 Ukuaji wa Mikopo kwa Sekta Binafsi	Asilimia	4.9	11.1	3.1	10.0	22.5	17.3	12.4	23.6
2.6 Uwiano wa Mikopo kwa Sekta Binafsi kwa pato la taifa[1]	Asilimia	14.3	14.6	14.0	14.3	16.0	17.0	17.4	21.6
2.7 Uwiano wa Mikopo kwa sekta binafSikwa mikopo yote	Asilimia	79.8	83.5	77.7	74.4	72.9	73.9	75.9	77.9
2.8 Riba za Amana za miezi 12	Asilimia	8.8	8.8	8.3	8.3	8.5	8.7	9.2	9.6
2.9 Riba za dhamana za serkali kwa ujumla	Asilimia	6.4	7.7	4.4	4.8	4.7	7.3	10.7	8.7
2.10 Riba ya mikopo ya muda mrefu hadi miaka mitano (3-5 years)	Asilimia	17.4	16.6	16.2	16.0	15.7	15.6	15.3	14.4
Mizania ya Malipo na Nchi za Nje									
3.1 Bidhaa Ziizouzwa Nje	Dola ya Marekani	4,292.7	5,377.6	6,371.7	6,756.2	7,223.8	7,696.6	9,121.6	10,293.6
3.2.Bidhaa Zilazoagizwa kutoka Nje ya Nchi	Dola ya Marekani	-8,519.7	-8,615.2	-7,831.7	-10,003.4	-14,208.7	-13,728.9	-14,195.6	-14,787.7
3.3.Urari wa Biashara	Dola ya Marekani	-4,227.0	-3,237.5	-1,460.0	-3,247.1	-6,984.9	-6,032.3	-5,074.0	-4,494.2
3.4.Urari wa Malipo ya Kawaida	Dola ya Marekani	-2,308.7	-1,340.2	-1,458.5	-2,374.3	-5,482.2	-2,960.6	-2,379.8	-2,015.2
3.5 Urari wa malipo yote	Dola ya Marekani	-784.0	587.0	-764.9	1,852.1	-988.4	52.3	70.1	968.9
3.6 Akiba ya Fedha za Kigeni	Dola ya Marekani	5,044.6	5,567.6	4,767.7	6,386.0	5,177.2	5,450.1	5,546.9	6,329.0
3.7 Akiba ya fedha za kigeni (miezi)	Miezi	4.9	6.4	5.6	6.6	4.7	4.5	4.5	4.9
3. 8 Kiwango cha kubadili fedha:									
Wastani wa mwaka	Thamani ya Tsh/Dola	2,263.8	2,288.2	2,294.1	2,297.8	2,303.1	2,382.1	2,597.4	2,537.6
Mwisho wa kipindi	Thamani ya Tsh/Dola	2,281.2	2,287.9	2,298.5	2,297.6	2,308.9	2,501.4	2,374.7	2,450.2
		2017/18	2018/19	2019/20	2020/21	2021/22	2022/23	2023/24	2024/25
Mwenendo wa Mapato na Matumizi									
4.1 Uwiano wa mapato ya ndani kwa Pato la Taifa[1]	Asilimia	14.8	14.3	15.0	13.7	14.9	15.0	14.7	15.6
4.2 Uwiano wa misaada kwa Pato la Taifa[1]	Asilimia	0.8	0.4	0.7	0.5	0.4	0.3	0.3	0.4
4.3 Uwiano wa Matumiazi ya kawaida kwa Pato la Taifa[1]	Asilimia	10.2	10.7	10.1	9.9	9.8	11.0	10.8	11.9
4.4 Uwiano wa matumizi ya maendeleo kwa Pato la Taifa[1]	Asilimia	6.6	6.5	7.1	7.8	9.2	7.4	7.2	6.9
4.5 Uwiano wa nakisi isiyo jumuisha misaada kwa Pato la Taifa[1]	Asilimia	-2.1	-2.9	-2.2	-4.0	-4.1	-3.4	-3.3	-3.2
4.6 Uwiano wa nakisi ya Jumla kwa Pato la Taita[1,2]	Asilimia	-1.9	-3.3	-1.9	-4.0	-3.6	-3.1	-3.1	-3.0
Deni la nje	Dola Milion	20,503.0	21,920.9	22,952.7	25,519.3	27,832.5	30,252.7	31,950.9	34,765.3
5.1 Mikopo ilyopokelewa	Dola Milion	18,765.1	20,029.3	20,958.4	23,250.9	25,392.8	27,889.3	30,416.1	34,053.0
5.2 Riba ambayo haijaipwa	Dola Milion	1,737.9	1,891.7	1,994.3	2,268.4	2,439.7	2,363.4	1,534.8	712.3

Chanzo:Wizara ya Fedha; Benki Kuu ya Tanzania; na Mamlaka ya Mapato Tanzania

Tanbihi:[1]Imetolewa kwa kuzingatia Pato la Tifa kwa bei za miaka husika; [2] inajumuisha misaada, matumizi yaliyochelewa (expenditure float), n.a-haipatikani, p, ni takwimu za muda.

Jedwali A2: Mwenendo wa Mapato na Matumizi ya Serikali – Tanzania Bara

Shilingi Milioni

	Bajeti ya	Julai 2026	
	2026/27	Makadirio	Halisi
Mapato ya ndani (yakijumuisha Mamlaka za Serikali za Mitaa)	46,228,159.4	3,198,357.3	3,502,199.3
Mapato ya Serikali Kuu	44,261,966.2	3,054,692.6	3,354,901.9
Mapato yatokanayo na kodi	37,246,376.1	2,574,527.2	2,877,009.9
Ushuru wa forodha	13,473,731.3	1,020,490.7	1,163,376.7
Kodi ya bidhaa na huduma	6,826,918.6	453,679.1	638,249.0
Kodi ya mapato	14,475,654.7	910,594.6	862,580.9
Kodi nyingine	2,470,071.5	189,762.8	212,803.3
Mapato yasiyotokana na kodi	7,015,590.1	480,165.4	477,891.9
Mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa	1,966,193.2	143,664.7	147,297.4
Jumla ya matumizi[1]	54,498,608.0	3,376,921.9	3,572,477.9
Matumizi ya kawaida	35,195,382.0	2,520,972.9	2,779,556.3
Mishahara	14,088,142.0	1,254,917.0	1,164,394.5
Malipo ya riba za mikopo	6,859,541.5	422,484.2	564,922.6
Ya ndani	4,030,300.9	192,158.5	383,781.9
Ya nje	2,829,240.6	230,325.7	181,140.8
Matumizi mengine ya kawaida	14,247,698.5	843,571.7	1,050,239.2
Matumizi ya maendeleo	19,303,226.0	855,949.0	792,921.5
Fedha za ndani	13,973,050.8	519,284.6	520,980.0
Fedha za nje	5,330,175.1	336,664.4	271,941.5
Nakisi ya bajeti bila ya misaada	-8,270,448.6	-178,564.6	-70,278.6
Misaada	563,139.4	103,464.9	75,694.1
Ya bajeti	0.0	0.0	0.0
Ya miradi	486,761.0	103,464.9	75,694.1
Ya kisekta	76,378.4	0.0	0.0
Nakisi ya bajeti ikijumuisha misaada	-7,707,309.2	-75,099.7	5,415.6
Marekebisho (Adjustments to cash and other items (net))	0.0	0.0	476,202.3
Balansi ya jumla	-7,707,309.2	-75,099.7	486,209.6
Ugharamiaji wa nakisi ya bajeti	7,707,309.2	75,099.7	-486,209.6
Ufadhili kutoka nje halisi	4,434,959.9	151,357.6	1,094,814.5
Mikopo	8,985,150.1	233,199.6	1,360,304.1
Mikopo ya bajeti	1,787,742.0	0.0	1,164,056.7
Mikopo ya miradi	7,140,971.1	233,199.6	196,247.4
ambayo: Mikopo ya masharti ya kibiashara	2,430,372.3	0.0	0.0
Mikopo ya kisekta	56,436.9	0.0	0.0
Marejesho ya mitaji ya mikopo ya nje	-4,550,190.2	-81,841.9	-265,489.6
Ufadhili wa ndani halisi[2]	3,272,349.3	-76,257.9	-1,581,024.1
Mikopo kutoka benki na vyanzo vingine	3,272,349.3	-76,257.9	-1,581,024.1
Mikopo ya benki	2,056,388.2	-63,692.3	-1,864,529.6
Mikopo toka vyanzo vingine (baada ya marejesho ya mitaji ya miko	1,215,961.2	-12,565.6	283,505.5
Mikopo ya ndani (rollover)	3,285,394.9	207,630.5	75,100.5
Kulipa mitaji ya mikopo ya ndani	-3,285,394.9	-207,630.5	-75,100.5

Chanzo : Wizara ya Fedha

Tanbihi: [1]Haijajumuisha marejesho ya mitaji ya mikopo na matumizi yaliyochelewa (expenditure float); [2]Thamani chanya ina maana ya ufadhili, na thamani hasi ina maana ya malipo au ongezeko la amana

Jedwali A3: Tathmini za Amana

Shilingi bilioni

Kipengele	Sep-25	Okt-25	Nov-25	Des-25	Jan-26	Feb-26	Mac-26	Apr-26	Mei-26	Jun-26	Jul-26	Ago-26	Sep-26
Rasilimali halisi za nje	15,896.7	15,715.4	16,298.6	15,286.5	15,950.0	15,749.5	15,245.6	14,553.5	13,309.2	13,449.0	14,646.0	13,575.4	13,152.3
Rasilimali halisi za nje za Benki Kuu	14,467.3	13,334.3	13,892.1	13,707.3	13,987.7	14,089.2	13,916.0	13,066.6	12,634.5	13,077.5	14,562.1	13,730.9	14,139.1
Rasilimali halisi za nje za mabenki	1,429.3	2,381.1	2,406.5	1,579.1	1,962.3	1,660.3	1,329.6	1,486.8	674.7	371.6	83.9	-155.5	-986.7
Rasilimali halisi za ndani	41,957.4	44,073.3	44,560.0	45,702.6	46,155.7	47,319.8	49,001.1	50,538.4	53,494.7	56,170.4	56,763.8	58,553.3	59,675.6
Madai ya ndani	54,854.2	56,509.3	57,629.3	57,229.9	57,872.1	58,896.1	59,877.3	61,759.8	63,283.0	65,928.9	65,914.8	68,093.2	69,436.3
Madai halisi kwa Serikali Kuu	12,854.4	14,122.4	14,243.8	12,626.9	12,700.8	12,841.9	12,660.8	13,840.5	14,248.3	14,005.8	12,141.2	12,837.3	13,076.9
Mikopo kwa sekta binafsi	41,999.9	42,386.9	43,385.5	44,603.1	45,171.4	46,054.2	47,216.5	47,919.3	49,034.6	51,923.1	53,773.6	55,255.9	56,359.4
Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3)	57,854.0	59,788.6	60,858.6	60,989.1	62,105.7	63,069.3	64,246.7	65,091.9	66,803.8	69,619.4	71,409.8	72,128.7	72,827.9
Fedha zilizo kwenye mzunguko	7,730.8	8,410.1	8,545.0	8,492.1	8,102.1	8,151.8	8,078.3	8,107.1	8,444.4	8,824.5	8,933.6	9,119.9	9,394.0
Amana za hundi	28,352.1	29,032.2	28,992.7	29,049.1	30,023.9	30,521.3	31,188.5	32,154.3	33,066.8	34,753.3	35,932.6	36,013.1	35,802.0
Amana za akiba na muda maalumu	21,771.2	22,346.4	23,320.9	23,447.8	23,979.7	24,396.2	24,979.9	24,830.5	25,292.6	26,041.5	26,543.6	26,995.7	27,631.8
Fedha taslim (M0)	13,717.6	15,068.7	15,135.7	14,508.3	15,225.1	14,990.0	14,998.9	15,670.5	15,640.3	16,738.8	16,188.3	17,245.9	17,127.7
Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3)	57,854.0	59,788.6	60,858.6	60,989.1	62,105.7	63,069.3	64,246.7	65,091.9	66,803.8	69,619.4	71,409.8	72,128.7	72,827.9
Amana za fedha za kigeni (FCD)	13,337.2	13,882.1	14,056.5	13,255.7	14,103.2	14,569.7	14,998.4	14,989.0	15,428.5	15,365.4	16,771.0	16,043.5	15,493.3
Amana za fedha za kigeni (Dola milioni)	*5,462.9*	*5,662.4*	*5,768.4*	*5,410.2*	*5,600.8*	*5,730.6*	*5,809.8*	*5,764.1*	*5,913.1*	*5,853.2*	*6,339.0*	*6,077.7*	*5,865.1*
Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana (M2)	44,516.8	45,906.5	46,802.2	47,733.4	48,002.5	48,499.6	49,248.3	50,102.9	51,375.3	54,254.1	54,638.9	56,085.2	57,334.6
Amana za akiba na muda maalum zilizo katika shilingi ya Kitanzania	16,600.4	16,848.4	17,618.1	17,919.5	18,229.5	18,541.9	19,071.4	18,951.4	19,122.7	19,982.0	19,984.5	20,492.4	21,212.9
Ujazi wa fedha, kwa tafsiri finyu (M1)	27,916.4	29,058.1	29,184.1	29,813.8	29,773.0	29,957.7	30,176.9	31,151.6	32,252.6	34,272.0	34,654.4	35,592.8	36,121.8
Fedha zilizo kwenye mzunguko	7,730.8	8,410.1	8,545.0	8,492.1	8,102.1	8,151.8	8,078.3	8,107.1	8,444.4	8,824.5	8,933.6	9,119.9	9,394.0
Amana za hundi	20,185.6	20,648.0	20,639.0	21,321.7	21,670.9	21,805.9	22,098.5	23,044.5	23,808.2	25,447.5	25,720.8	26,472.9	26,727.7

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

Jedwali A4: Muundo wa Viwango vya Riba

Asilimia

Kipengele	2025 Sep	Okt	Nov	Des	2026 Jan	Feb	Mac	Apr	Mei	Jun	Jul	Ago	Sept
A: Riba za mikopo/amana zilizo katika shilingi													
1. Riba katika soko la fedha baina ya mabenki													
Siku 1 (*Overnight*)	6.29	6.45	6.08	6.00	6.13	6.01	6.17	6.15	5.94	5.53	5.92	6.37	6.26
Siku 2-7	6.43	6.29	6.19	6.30	6.34	6.31	6.25	6.18	5.96	5.90	6.23	6.45	6.56
Siku 8-14	6.93	6.92	6.84	6.26	6.74	6.83	6.53	6.33	6.48	6.46	6.90	7.09	7.06
Siku 15-30	7.35	7.07	7.23	6.40	7.06	6.96	6.85	6.79	6.58	6.64	7.31	6.95	6.83
Siku 31-60	7.50	7.28	7.00	7.20	7.23	7.00	7.20	6.92	6.79	6.70	6.90	6.91	6.96
Siku 61-90	9.14	9.14	7.00	8.11	9.96	7.00	8.50	7.12	6.79	6.84	6.82	7.07	7.07
Siku 91-180	7.00	9.75	8.89	8.89	6.75	7.00	8.07	8.77	7.27	7.07	6.92	7.94	7.08
Zaidi ya siku 180	10.93	10.93	10.93	10.93	10.93	12.00	12.00	12.00	12.00	12.00	12.00	12.00	12.00
Riba ya jumla	6.45	6.38	6.30	6.29	6.40	6.34	6.32	6.26	6.14	6.00	6.57	6.67	6.67
2. Riba ya mikopo ya siku 1 kati ya mabenki na	7.75	7.75	7.75	7.75	7.75	7.75	7.75	7.25	7.25	7.25	7.75	7.75	7.75
3. Riba ya mikopo ya muda mfupi toka kwa	4.79	4.79	4.79	5.75	5.75	5.75	5.75	5.75	5.75	5.75	6.25	6.25	6.25
4. Riba ya mikopo ya muda mfupi kwa	5.76	5.76	5.77	5.75	5.75	5.75	5.75	5.75	5.75	5.75	6.25	6.25	6.25
5. Riba ya dhamana za serikali													
Siku 35	6.20	5.94	5.64	5.38	5.36	4.75	4.20	3.81	3.23	2.82	2.34	2.11	2.41
Siku 91	6.81	6.21	6.08	5.93	5.73	4.97	4.23	4.02	3.78	3.56	3.40	3.42	3.40
Siku 182	6.56	6.41	5.92	5.91	5.85	5.85	5.69	5.46	5.23	4.98	4.74	5.12	5.11
Siku 364	5.99	6.00	6.45	6.24	6.21	6.20	5.80	5.72	5.63	6.65	7.07	6.70	6.38
Riba ya jumla	6.03	6.27	6.25	5.87	5.89	5.68	5.21	5.06	4.74	4.83	4.74	4.86	4.85
6. Riba za hati fungani za serikali													
Miaka miwili	12.17	10.05	10.05	10.05	10.05	10.05	8.36	8.36	8.36	8.36	8.40	8.40	8.40
Miaka mitano	12.48	12.48	10.54	10.54	10.54	10.54	10.54	9.54	9.54	9.54	9.54	9.54	9.53
Miaka saba	9.71	9.71	9.71	9.71	9.71	9.71	9.71	9.71	9.71	9.71	9.71	9.71	9.71
Miaka kumi	13.74	12.45	12.45	12.45	11.30	11.30	11.30	9.40	9.40	10.39	10.87	10.87	10.69
Miaka kumi na tano	13.91	13.91	12.08	12.08	12.08	10.78	10.78	10.78	10.39	10.39	10.39	10.55	10.79
Miaka ishirini	13.55	13.55	13.55	12.02	12.02	12.02	10.71	10.71	10.43	10.43	11.33	11.33	11.33
Miaka ishirini na tano	13.19	13.19	13.19	13.19	13.19	11.99	11.99	11.99	11.99	11.89	11.89	11.48	11.48
7. Riba inayotumika kutathmini dhamana	8.25	8.25	8.25	8.25	8.25	8.25	8.25	8.25	8.25	8.25	8.75	8.75	8.75
8. Riba za amana za akiba	2.92	2.93	2.88	3.02	2.94	2.98	2.89	2.91	2.85	2.90	2.90	2.77	2.95
9. Riba za jumla za amana za muda maalum	8.50	8.36	8.54	8.36	8.33	8.32	8.33	8.54	8.43	8.69	8.78	8.78	9.03
Mwezi 1	9.65	9.10	9.31	9.35	8.96	9.10	8.65	9.06	8.34	9.28	9.51	9.41	9.71
Miezi 2	9.28	10.09	9.67	9.34	9.56	9.16	9.34	9.67	8.65	9.84	10.13	10.08	9.89
Miezi 3	9.61	9.38	9.42	9.70	9.43	9.03	9.56	9.01	10.52	9.96	9.61	9.74	10.19
Miezi 6	10.12	10.06	10.01	9.96	10.20	10.26	10.51	10.35	9.87	10.46	10.54	10.56	10.47
Miezi 12	9.84	9.21	10.02	9.58	9.70	9.82	9.60	9.81	10.17	9.72	9.34	9.36	9.59
Miezi 24	7.63	7.05	7.92	7.21	7.11	7.35	7.03	8.20	7.69	7.91	7.91	7.97	8.81
10. Riba za amana kwa wateja wakubwa	11.05	11.22	11.67	11.66	11.74	11.48	11.57	11.37	11.25	11.17	10.99	11.06	11.00
11. Wastani wa riba za mikopo	15.18	15.19	15.27	15.24	15.10	15.11	15.11	15.33	15.32	15.22	15.10	15.05	15.54
Muda mfupi (Hadi mwaka 1)	15.52	15.50	15.53	15.46	15.49	15.41	15.45	15.31	15.38	15.38	15.54	15.31	15.36
Muda wa kati (Mwaka 1 hadi 2)	16.26	16.42	16.42	16.42	16.73	16.70	16.53	17.19	17.11	17.10	16.51	16.53	16.88
Muda wa kati (Miaka 2 hadi 3)	15.19	15.13	15.18	15.43	14.97	15.27	15.31	15.63	15.60	15.19	15.11	15.02	16.02
Muda mrefu (Miaka 3 hadi 5)	14.26	14.24	14.43	14.29	14.05	13.96	13.95	14.56	14.43	14.38	14.44	14.44	15.14
Muda mrefu (Zaidi ya Miaka 5)	14.66	14.68	14.79	14.61	14.24	14.20	14.30	13.96	14.08	14.03	13.92	13.93	14.31
12. Riba za mikopo kwa wateja wakubwa	12.84	12.40	12.61	12.38	12.25	12.19	12.21	12.56	11.90	11.93	12.04	11.93	12.03
B: Fedha za kigeni													
1. Riba za amana													
Amana za akiba	0.98	1.75	0.57	0.87	0.77	0.70	1.22	1.68	1.06	1.64	1.65	1.80	1.41
Riba za jumla za amana za muda maalum	3.94	4.17	4.03	3.67	4.18	4.29	4.26	4.41	4.47	4.30	4.11	4.12	4.14
Mwezi 1	2.46	2.44	2.45	2.45	2.52	2.45	2.47	3.42	2.52	2.49	2.49	2.46	2.49
Miezi 2	4.98	4.93	6.12	2.96	4.97	4.85	4.84	3.91	4.05	5.02	4.72	3.34	3.63
Miezi 3	2.56	4.55	2.87	4.92	4.95	4.94	4.69	4.87	5.03	4.72	3.94	4.84	4.72
Miezi 6	5.10	5.05	5.25	4.82	4.66	4.80	4.97	5.03	5.14	4.69	4.76	4.64	4.73
9 months	4.61	3.86	3.47	3.19	3.82	4.43	4.35	4.83	5.59	4.57	4.65	5.31	5.10
Miezi 12	8.43	8.71	8.52	8.61	8.57	8.61	8.70	8.96	8.72	9.03	8.88	8.96	9.17
Muda mfupi (Hadi mwaka 1)	9.89	9.88	9.89	9.91	10.00	10.00	10.00	10.07	9.95	9.99	10.02	10.03	10.51
Muda wa kati (Mwaka 1 hadi 2)	7.49	7.73	7.65	7.68	7.68	7.72	7.69	8.82	7.88	8.31	8.13	8.35	8.61
Muda wa kati (Miaka 2 hadi 3)	7.25	7.43	7.49	8.31	8.35	8.23	8.19	8.64	7.79	8.84	8.81	8.70	9.02
Muda mrefu (Miaka 3 hadi 5)	9.16	9.23	9.30	8.50	8.64	8.83	9.09	9.19	9.08	9.09	8.70	8.74	8.80
Muda mrefu (zaidi ya miaka 5)	8.35	9.28	8.28	8.66	8.17	8.28	8.50	8.09	8.88	8.92	8.76	8.96	8.92

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

Jedwali A5: Mizania ya Malipo ya Nje

Dola za Marekani Milioni

	2021	2022	2023	2024	2025
A. Urari wa malipo ya kawaida	-2,374.3	-5,482.2	-2,960.6	-2,379.8	-2,049.4
Bidhaa: zilizouzwa nje ya nchi (f.o.b)	6,756.2	7,223.8	7,696.6	9,121.6	10,262.9
Bidhaa asilia	627.9	766.5	953.3	1,473.3	1,491.9
Bidhaa zisizo asilia	5,763.0	6,058.4	6,321.6	7,228.8	8,464.5
kati ya hizo: Dhahabu	2,737.1	2,835.1	3,058.9	3,419.6	4,753.9
Bidhaa zisizo rekodiwa	365.4	399.0	421.6	419.6	306.6
Bidhaa: zilizoagizwa kutoka nje ya nchi (f.o.b)	-10,003.4	-14,208.7	-13,728.9	-14,195.6	-14,787.7
Urari wa biashara ya bidhaa	-3,247.1	-6,984.9	-6,032.3	-5,074.0	-4,524.8
Huduma: mapato	3,117.7	4,762.0	6,231.7	6,846.8	7,477.5
Usafirishaji	1,558.1	1,872.0	2,333.4	2,353.4	2,647.6
Utalii	1,310.3	2,527.8	3,373.8	3,903.1	4,410.6
Nyingine	249.3	362.2	524.4	590.3	419.2
Huduma: malipo	-1,607.0	-2,465.4	-2,395.9	-2,795.0	-3,241.8
Usafirishaji	-806.4	-1,378.4	-1,326.4	-1,411.9	-1,467.3
Utalii	-196.2	-357.5	-477.2	-522.3	-715.5
Nyingine	-604.4	-729.5	-592.3	-860.9	-1,059.1
Urari wa biashara ya huduma	1,510.7	2,296.6	3,835.9	4,051.7	4,235.7
Urari wa biashara ya bidhaa na huduma	-1,736.4	-4,688.3	-2,196.5	-1,022.3	-289.1
Mapato ya vitega uchumi: yaliyoingia	102.5	183.9	301.2	311.7	306.2
Malipo ya vitega uchumi: yaliyotoka	-1,294.2	-1,577.1	-1,797.7	-2,199.2	-2,356.3
Urari wa mapato ya vitega uchumi	-1,191.6	-1,393.2	-1,496.6	-1,887.4	-2,050.1
Urari wa bidhaa, huduma na mapato ya vitega uchumi	-2,928.0	-6,081.5	-3,693.1	-2,909.7	-2,339.2
Mapato ya uhamisho mali wa kawaida: yaliyoingia	640.1	716.5	1,280.9	1,177.4	899.1
Serikali	104.7	76.4	131.0	139.2	19.7
Taasisi za zisizo za serikali	535.4	640.2	1,150.0	1,038.3	879.4
Malipo ya uhamisho mali wa kawaida: yaliyotoka	-86.4	-117.2	-548.4	-647.5	-609.2
Urari wa uhamisho mali wa kawaida	553.7	599.3	732.5	529.9	289.9
B. Urari wa uhamisho mitaji	412.1	274.0	223.4	318.7	348.9
Uhamisho wa mitaji: ulioingia	412.1	274.0	223.4	318.7	348.9
Serikali	346.8	208.7	158.0	253.3	289.8
Taasisi za zisizo za serikali	65.3	65.3	65.3	65.3	59.1
Uhamisho wa mitaji: uliotoka	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0
Jumla, A na B	-1,962.1	-5,208.2	-2,737.2	-2,061.1	-1,700.5
C. Urari katika uwekezaji	4,037.1	3,634.7	3,629.9	1,857.4	2,750.0
Uwekezaji wa moja kwa moja	1,190.5	1,437.6	1,648.9	1,656.0	1,850.4
Uwekezaji wa hisa	-7.9	24.6	13.9	10.6	82.3
Uwekezaji mwingine	2,854.5	2,172.5	1,967.1	190.7	817.3
Mali (assets)	-89.8	193.0	-749.6	-924.6	-417.3
Madeni (liabilities)	2,944.3	1,979.6	2,716.6	1,115.3	1,234.6
Jumla, makundi A hadi C	2,074.9	-1,573.4	892.7	-203.8	1,049.5
D. Makosa na masahihisho	-222.8	585.0	-850.8	273.9	-80.6
Urari wa malipo yote	1,852.1	-988.4	41.9	70.1	968.9
E. Akiba ya fedha za kigeni	-1,852.1	988.4	-41.9	-70.1	-968.9
Vipengele vya kumbukumbu					
Uwiano wa urari wa malipo ya kawaida kwa pato la taifa	-3.4	-7.1	-3.7	-2.9	-2.2
Akiba ya fedha za kigeni	6,386.0	5,177.2	5,450.1	5,546.9	6,329.0
Akiba ya fedha za kigeni (miezi ya uagizaji wa bidhaa nje)	6.6	4.7	4.5	4.5	4.9
